# Nipashe

Jumatano Novemba 11, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580396

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




**NDUGU** wawili washambuliwa kwa mapanga, mmoja auawa

UKURASA 4



**MWALIMU** taaluma adaiwa kumbaka mwanafunzi wake

UKURASA 3

**Makocha EPL wataka 'sab' wachezaji wa5**

UKURASA 20

# Spika aonya wabunge kukopeshana fedha

• **Asema** hatahusika na yatakayotokea, asisitiza Bunge la 12 halitakuwa la 'Ndiyo Mzee... *Endelea ukurasa 2*



Mbunge wa Kongwa, Job Ndugai, akila kiapo baada ya kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la 12 jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**COMORO YAPONGEZA UCHAGUZI TANZANIA**

RAIS wa Visiwa vya Comoro, Azali Assouman, ameipongeza Tanzania kwa kufanya uchaguzi huru...

## Serikali yadhibiti wauza saruji kwa bei juu

UKURASA 3



# ...JPM awapa meno kuwabana mawaziri

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

SALAMU ZA PONGEZI



Gazeti Nipashe linampongeza Rais Dkt John Magufuli na Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha Miaka 5. 2020 - 2025

Kwa salamu za pongezi

Wasiliana nasi kwa Simu: 0686 101335

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz



SALAMU ZA PONGEZI

# Spika awaonya wabunge kukopeshana kinyemela

**Na Romana Mallya,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amewatahadharisha wabunge walioanza kikao jana kuwa makini dhidi ya wenzao watakaojitokeza na hitaji la kutaka kukopa fedha kwao, kwamba ni makubaliano yaliyosheheni matatizo.

"Sikupaswa kulisema hili lakini mniwie radhi niliseme tulipata tabu sana kwenye Bunge lililopita... Kwa hiyo, mkikopeshana huko, mimi simo, toka asubuhi atakuja mtu na lugha nzuri sana, siyo kweli unaingia mkenge."

Ndugai alitoa kauli hiyo bungeni jijini hapa jana, ukiwa ni ujumbe wake mahususi baada ya kuwawasilishia wabunge miongozo rasmi, akisisitiza ni jambo linaloleta usumbufu mkubwa ambao safari hii hatakuwa tayari kuwajibika nao.

Hata hivyo, Spika Ndugai hakufafanua kwa kina namna mikasa hiyo ilivyo, idadi ya matukio na sura yake pana, ingawa katika kauli ya mjumuisho, alilipa sura yenye uzito mkubwa.

Vilevile, Spika Ndugai aliahidi taarifa za Bunge la 12 zitasikika kwa mawanda mapana katika nyenzo za vyombo vya habari, akisisitiza umuhimu wa taarifa hizo kuonekana na kusikika kwa kadri inavyostahili, wabunge wanavyoishauri serikali yao.

"Tunaviomba vyombo vya habari mtoe taarifa ziwafikie wananchi. Tukijifungia hapa habari zisiwafikie wananchi, Bunge litakuwa limehukumiwa toka mwanzo kwa sababu lina wabunge wengi wa CCM, ndiyo maana halisikiki, halifanyi kazi, halionekani.

"Mlio wengi mkichagua wachache wasikike, 'itakula kwenu'. Niwaombe wabunge mzipitie kwa makini kanuni, lakini baada ya Bunge, zitafanyika semina mbalimbali.

"Mzingatie mavazi hususani kinamama, hata kwa wageni mnaokuja bungeni mzingatie hili. Waliolikosa Bunge, 'wanapamisi' hapa kweli kweli," alisema.



Mwenyekiti wa CCM, Rais Dk. John Magufuli, akizungumza na wabunge wateule wa chama hicho, katika ukumbi wa White House, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IKULU**

# Magufuli awataka wafoke bungeni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, ametoa maagizo kadhaa kwa wabunge wa chama hicho, ikiwa ni pamoja na kuwajibika ipasavyo bungeni hata ikiwezekana kufoka.

Akizungumza juzi na wabunge wateule wa CCM, Makao Makuu ya chama hicho jijini hapa, Dk. Magufuli alisema ushindi uliopatikana ni mkubwa lakini wasijisahau.

"Mara nyingi watu mnapokuwa na ushindi mkubwa inawezekana tukaanza kujisahau na tumeahidi mambo mengi wakati tukiomba kura, yapo tuliyahidi viongozi wa kitaifa, yapo yaliyoahidiwa kwenye Ilani ya CCM yenye kurasa 303, lakini yapo ambayo ninyi waheshimiwa wabunge mmeyaahidi katika maeneo yenu," alikumbusha.

Alisema wabunge hao wana wajibu mkubwa wa kuyatekeleza kwa sababu ahadi huwa ni deni.

"Sasa, mimi niwaombe waheshimiwa wabunge kwa vile tulichoomba tumekipata, sasa ni wajibu wetu kutumiza yale tuliyokuwa tumeyaahidi kwa wananchi.

"Mara nyingi katika uzoefu wangu miaka mitano iliyopita tunapoenda kule wilayani vijijini na mikoani pamekuwa na kero nyingi za watu ambazo watu wamekuwa wakilalamika.

"Unasimama tu kidogo unakuta hasa kinamama na watoto, sasa niwaombe kwa vile mliahidi kutekeleza kero za wananchi na ndiyo ahadi ya chama chetu katika ilani ya uchaguzi ya mwaka huu, kila mmoja wetu kwanza tukajipange kutembelea majimbo yetu, kazi ya mbunge ni jimbo, na jimbo lazima alijue," alisema.

Dk. Magufuli alisema kama wabunge hao wanataka kukaa muda mrefu kwenye majimbo, lazima wayatambue vizuri.

"Niwaombe sana, teteeni vizuri majimbo yenu, semeeni majimbo yenu hata kama ni kufokafoka, ili waziri akishindwa kujibu hoja zake, ni yeye mwenyewe waziri, lakini msiende 'beyond the border' (msivuke mipaka), saa nyingine tunapigana vita sisi wenyewe," alisema.

Aliwataka wabunge hao kwenda kuimarisha umoja wao ndani na nje ya Bunge na kuisimamia ipasavyo serikali atakayoiunda kwa maslahi ya taifa.

Vilevile, aliwapongeza wabunge wateule wanawake kwa kuongezeka idadi yao katika Bunge na kuwataka kwenda kuwatetea wanawake wanyonge.

"Mkawe sauti yao na mimi ninawaahidi nitaendelea kuteua wanawake," alisema.

Awali, chama hicho kilifanya mafunzo ya kimkakati kuhusu nafasi ya wabunge wa CCM katika kusimamia maslahi ya taifa wawapo bungeni huku msisitizo ukiwekwa katika kusimamia umoja na heshima ya chama unaojengwa na uadilifu wa wabunge hao.

Mafunzo hayo yaliendeshwa Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Philip Mangula na Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk. Bashiri Ally.

## ... Asema halitakuwa Bunge la 'Ndiyo Mzee'

**Na Romana Mallya**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ameahidi kulifanya Bunge jipya kuwa lililojaa udadisi, akiwahimiza wajumbe wake kamwe kutoishia kuwa waitikia wa 'ndiyo' au 'hapana' pekee.

Sambamba na hilo, Spika Ndugai amewahakikishia haki zao wabunge wachache waliopo kutoka upinzani, akiwataka wawajibike kwa kadri wanavyostahili ili kulipa Bunge uhai sahihi wa kuutumikia umma.

"Wabunge wengi ni kweli wanatoka CCM. Hii haimaanishi Bunge kuwa la 'ndiyo... ndiyo...' au 'hapana... hapana...' litatekeleza wajibu wake kama ipasavyo.

"Miongoni mwetu mtateuliwa kuwa mawaziri na manaibu waziri, niwahakikishie mtawajibika kweli, hakuna kubebana," Ndugai alitahadharisha.

Katika wosia aliowalenga zaidi wabunge wageni, akiwadokeza dhana asiyokubaliana nayo kama vile kuwapo aliowaita 'wabunge bubu' na 'wanaojipendekeza', akiwakumbusha wote kuwa tija ya kazi yao hatima yake iko kwa wananchi watakaporudi kwao.

"Ukichagua kuwa mbunge bubu, husemi, upoupo tu, eti uonekane una nidhamu kwenye chama au mahali kwingine, 'umeliwa', huo ndiyo ukweli!" Spika Ndugai alisema na kuongeza:

"Utakuwa umejimaliza, ukidhani kunyamaza ndiyo nidhamu, wananchi wamekuchagua kwa sababu wanaamini uwezo wa kuwasemea mambo yao kuiambia serikali."

Awali, Ndugai, Mbunge wa Kongwa mkoani Dodoma, alichaguliwa tena jana kuwa Spika wa Bunge, akishinda kwa kupigiwa kura za wajumbe wote kasoro mmoja walioshiriki kikao cha kwanza cha Bunge hilo la 12.

Kabla ya Mwenyekiti wa Muda, William Lukuvi, kumtangaza mshindi kwa kupata kura za wajumbe 345, Ndugai alijinadi kwa dakika tatu, akiwasilisha ahadi aliyotamka: "Nitawatendea haki wabunge wote, nitalifanya Bunge hili la 12 liwe Bunge la mfano, ambalo halijawahi kupatikana toka uhuru wa nchi.

"Kama mbunge mwenzenu, ninaelewa sana matatizo ya wabunge, madhila, wapi panabana na katika mambo muhimu yale nitakuwa mstari wa mbele, ninafikiri tunaelewana!"

Vilevile, katika uwasilishaji wake huo, Ndugai aliwageukia wabunge wa upinzani akiwaomba ridhaa yao kwa kauli ya ujumbe mahususi kwamba: "Mtaishi kwa raha bila tatizo lolote, hamtabaguliwa na mtafanya kazi yenu vizuri.

"Watanzania watarajie Bunge ambalo litawapa matokeo mazuri na mwisho mtakubali Bunge la 12 limewatumikia. "Pamoja na kanuni kutamka nije kukalia kiti hiki kwa ajili ya uchaguzi wa Spika wa Bunge, mngeweza kupinga lakini mmekubali bila kupinga," alitamka Ndugai katika salamu zake za shukurani.

Awali, Katibu wa Bunge, Stephen Kagaigai, akisoma tangazo la Rais John Magufuli, alisema kikao hicho ni haki rasmi ya kikatiba aliyonayo mkuu wa nchi.

# Walanguzi saruji wadhibitiwa

**Na Mwandishi Wetu**

BEI ya saruji katika eneo la Ngorongoro na Loliondo, mkoani Arusha hadi jana kwa mfuko mmoja wa kilo 50, iliuzwa kwa Sh. 23,000.

Uchunguzi wa Nipashe katika maeneo hayo ambayo katika taarifa yake ya juzi iliripoti kuuzwa hadi Sh. 35,000, ulibaini kuwa bei hiyo ilikuwa inauzwa kwenye duka moja ambalo mfanyabiashara mmoja aliamua kuuza kwa bei ya ulanguzi.

"Mimi nanunua saruji Sh. 24,000 hadi 25,000 napeleka Loliondo kwenye kijiji cha Soiti Sambu, lilipo duka langu ni mbali ukijumlisha gharama za usafiri, nauza kwa 35,000 ili nipate faida," alisema mfanyabiashara huyo.

Baada ya bei hiyo ya Sh. 35,000 kwa mfuko wa kilo 50 kuibua taharuki, Nipashe ilifuatilia kwa waagizaji wa bidhaa hiyo kwenye baadhi ya maduka mkoani humo ambao walisema mfuko mmoja unanunuliwa kwa Sh. 17,000 jijini Arusha na ukisafirishwa hadi Ngorongoro na Loliondo unauzwa kwa Sh. 23,000.

"Bei ya leo asubuhi dukani ni Sh. 23,000, ikipanda sio zaidi ya Sh. 25,000," alisema mmoja wa wauzaji wa bidhaa hiyo ambaye hakupenda jina lake litajwe gazetini.

Taarifa ambazo Nipashe imezipata jana ni kuwa mamlaka zimeingilia kati kuhakikisha bidhaa hiyo haiuzwi zaidi ya Sh. 17,000 kwa mfuko mmoja.

Aidha, wafanyabiashara wanaozidisha bei ya bidhaa hiyo wameonywa.

Katika baadhi ya maeneo nchini kumekuwa na ongezeko la kati ya Sh. 5,000 hadi Sh. 3,000 kwa mfuko mmoja wa kilo 50.

**TANGA**

Lulu George kutoka Tanga anaripoti kuwa Mkuu wa Mkoa huo, Martine Shigela, amewaagiza watendaji wake kuhakikisha wanakagua maduka ili kuwabaini wafanyabiashara waliopandishaji bei ya saruji.

Shighela amesema wafanyabiashara watakaobainika kuhusika na ulanguzi huo, wachukuliwe hatua kali za kisheria ikiwa ni pamoja na kuwafutia leseni za biashara.

Alitoa agizo hilo jana alipozungumza na waandishi wa habari kwenye Kiwanda cha Saruji cha Kilimanjaro na Simba alikozuru kikazi kujionea uzalishaji wa bidhaa hiyo muhimu.

Shighela aliagiza wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri, maofisa biashara, maofisa tarafa, watendaji wa kata na wenyeviti wa vijiji kuhakikisha wanasimamia suala hilo.

Alisema kupungua kwa uzalishaji wa saruji kulikosababishwa na maboresho ya viwanda, kusiwe sababu ya kuongeza bei ya bidhaa hiyo sokoni, hivyo hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya wafanyabiashara waliopandisha bei ya saruji.

"Ninawaagiza watendaji wa serikali wakiongozwa na wakuu wa wilaya, kukagua kwenye maghala yote na iwapo yupo mfanyabiashara ameongeza bei, asiachwe, afutiwe leseni na akatafute shughuli nyingine ya kufanya," alionya.

Alibainisha kuwa katika viwanda vyote alivyotembelea, amebaini hakuna ongezeko lolote la gharama za uzalishaji wa saruji na kwamba bei ya bidhaa hiyo kiwandani bado ni ileile ya siku zote.

"Wafanyabiashara ndiyo wameongeza bei kwenye soko lakini viwandani bado bei ni ileile, sasa katika hili hatuna mchezo nalo, wafanyabiashara wajiangalie sana," alionya.

Hata hivyo, aliwataka wenye viwanda kuongeza uzalishaji wa bidhaa hiyo hasa kwa kuzingatia kuwa mahitaji ya bidhaa hiyo bado ni makubwa hususan kipindi hiki ambacho serikali ipo katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo.

Mkurugenzi Mkazi wa Simba Cement, Benedict Lema, alisema kiwanda hicho kimeendelea na uzalishaji na kwamba mwezi uliopita walivuka lengo la uzalishaji na kufikia tani 108,000 toka tani 107,000 walizokuwa wamejipangia.

"Kwa muda wa siku saba tumepumzisha mashine lakini bado tumeuza tani 2,002 na ukweli ni kwamba hatujaongeza bei ya saruji hata kidogo wala gharama za uzalishaji hazijaongezeka," alisema Lema.

Msimamizi Mkuu wa Fedha katika Kiwanda cha Kilimanjaro Cement, Philbert Nshange, alisema kiwango cha uzalishaji kwa siku kiwandani hapo ni tani 300.

Alibainisha kuwa bei ya saruji kwa viwandani ni kuanzia Sh. 11,600 hadi Sh. 12,000 kwa mfuko mmoja wa Kg 50.




Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martin Shigela (wa pili kushoto), akipokea maelezo ya bei ya saruji kutoka kwa Msimamizi wa Fedha wa kiwanda cha Tanga Cement, Isaac Lupokela (kushoto), alipotembelea kiwandani hapo jana. Watatu kushoto ni Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Benedict Lema. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Mwalimu taaluma adaiwa kumbaka mwanafunzi wake

**Na Christina Haule,** MOROGORO

JESHI la Polisi mkoani hapa, linamshikilia Mwalimu wa Shule ya Msingi Montfort iliyoko Kola B, Manispaa ya Morogoro, Eneza Anderson (27), mkazi wa Kihonda Maghorofani kwa tuhuma za kumbaka mwanafunzi wake wa darasa la tano.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, tukio hilo liliripotiwa polisi Novemba 5, mwaka huu, majira ya saa 6:00 mchana.

Mutafungwa alisema mtuhumiwa huyo anadaiwa kuwa alimbaka mwanafunzi huyo mwenye umri wa miaka 10 (jina linahifadhiwa).

Kamanda Mutafungwa alisema mwanafunzi huyo alipohojiwa alidai kuingiliwa kimwili na mwalimu wake mara kadhaa kwenye maeneo ya ofisini na chooni wakati wanafunzi wenzake wanapokuwa darasani.

Alisema kwa mujibu wa taarifa kutoka katika ofisi za dawati la jinsia na watoto mkoani Morogoro, mtuhumiwa huyo ni mwalimu wa taaluma katika shule hiyo.

Mutafungwa alisema Jeshi la Polisi lilimhoji mtuhumiwa katika hatua ya awali na kukiri kumbaka na kumlawiti mwanafunzi mara tano.

Kamanda Mutafungwa alisema hatua za kumfikisha mahakamani kwa kushirikiana na maofisa ustawi wa jamii zitafuata baada ya upelelezi kukamilika.


## BANI INVESTMENT LIMITED
### DEBT COLLECTORS/ AUCTIONEERS

### TANGAZO LA MNADA

Kwa idhini tuliyopewa na **BENKI YA NBC MAKAO MAKUU** tunatoa notisi ya siku 14 na tangazo la mnada wa hadhara wa mali zilizoorodheshwa hapo chini ambazo ziliwekwa kama dhamana ya mkopo. Hivyo basi utakapopita muda wa siku kumi na nne tangu kutoka kwa gazeti hili, Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada.Mnada utafanyika mahali zilipo mali hizi, kama ilivyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:-

| JINA LA AKAUNTI | MMILIKI | MALI ZILIZOWEKWA DHAMANA | MAHALI |
|---|---|---|---|
| ABUBAKARY SAID SEIFU | ABUBAKARY SAID SEIF | Nyumba yenye CT NO.20282-DLR, LO NO.96253/15859, PLOT NO.81, BLOCK 'G' | NKUHUNGU NORTH-DODOMA |
| BAHATI S. MANYAMA | BAHATI SENGELEMA MANYAMA | Nyumba yenye CT NO.24768-LR MWANZA, LO NO.388664, PLOT NO.353, BLOCK "E" | MAJENGO - KAHAMA |
| MINYARO LUSHANGA SHIJA | BUHOLO LUSHANGA | CT NO.23700-LR MWANZA, L.O.NO.388591 PLOT NO. 24 | MBULU AREA, KAHAMA |
| MMETA KAOMBWE SAIDI | MMETA SAID KAOMBWE | Nyumba yenye C.T NO. 24918 - LR MWANZA, L.O NO. 370508 PLOT NO. 896, BLOCK 'RR' | CHEMCHEM AREA, TABORA |
| FRIDA FURNITURE | JUVENALI SHABANI SHILYANGA | Nyumba yenye C.T NO. 20703 LR MWANZA L.O NO. 156243 PLOT NO. 320 BLOCK 'V' | MWANZA |
| JUSTINE WEREMA MARWA | JUSTINE WEREMA MARWA | Nyumba yenye CT NO. 25321-LR MWANZA, L.O. NO. 366528, PLOT NO. 507, BLOCK 'G' | BOMANI AREA TARIME |
| YAGESA M. NGOMA | YAGESA MAKUNGWI NGOMA | Nyumba yenye CT.NO. 26826,L.O NO 200840, PLOT.NO.21, BLOCK 'A' HD | DIDIA - SHINYANGA |
| KITWAN MIRAMBO | Kitwan Kasongo Mirambo | Nyumba yenye CT NO. 47080-LR MWANZA, L.O. NO. 479617, PLOT NO. 85, BLOCK 'E' | MWANZA ROAD, TABORA |
| HAMIS KOMBO | HAMIS KOMBO | Nyumba yenye CT.NO. 35430-LR MWANZA, L.O NO. 423417, PLOT.NO. 36, BLOCK 'GG' | KITANGIRI - SHINYANGA |
| JULIUS MAFURU MHOJI | JULIUS MAFURU | Nyumba yenye CT NO. 21168-LR MWANZA, L.O. NO. 301722, PLOT NO.762, BLOCK 'HH' | NYAKATO-MWANZA |
| MASUDI OMARI OTHMANI | MASUDI OMARY OTHUMANI | Nyumba yenye C.T NO. 22035- LR MWANZA, L.O NO. 229290, PLOT NO. 19, BLOCK 'EE' | MABATINI - TABORA |
| EMMANUEL G GAMBI | EMMANUEL GODWIN GAMBI | Nyumba yenye CT NO. 114903, LO. NO. 395223,PLOT NO, 68,BLOCK 'Q' | KIBAMBA-DAR ES SALAAM |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mali zitauzwa "kama zilivyo " as is where is basis"
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada na kiasi kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwa hapo juu hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki ni juu ya mnunuzi
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wowote isipokuwa usiku.

215989902

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na Ofisi ya:**
**Kwa maelezo zaidi wasiliana Na ofisi ya BANI INVESTMENT LTD Nkurmah Street, Lida Building, Ghorofa ya 3, Chumba No. 0313 S.L.P 71340 Dar es Salaam au kwa simu na. 0713 224578, 0622 020147, 0653 640999**

# Ndugu wawili washambuliwa kwa mapanga, mmoja auawa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKAZI wa Mamba Lekura, Moshi mkoani Kilimanjaro, Evarist Meena, anadaiwa kuuawa kwa kushambuliwa kwa mapanga na watu wasiojulikana wakati ndugu yake, Eden Meena akijeruhiwa vibaya.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi (ACP) Emmanuel Lukula, alisema jana kuwa watu hao ambao ni ndugu wa familia moja, walivamiwa na kukatwakatwa sehemu mbalimbali za miili yao wakiwa eneo la Marangu Mtoni.

Kwa mujibu wa Kamanda Likula, alisema tukio hilo lilitokea usiku wa Novemba 6, mwaka huu, na kuongeza kuwa polisi wanaendelea na uchunguzi ili kubaini chanzo chake.

"Kuna tukio la ndugu wawili wa familia moja kukatwa mapanga na mmoja kupoteza maisha. Ingawa mtu aliyefanya tukio hilo alifahamika na inadaiwa amekimbilia nchi jirani, jitihada zinaendelea ili kuhakikisha anakamatwa ili kufikishwa mbele ya sheria," alisema Kamanda Lukula

Hata hivyo, baadhi ya shuhuda wa tukio hilo, Bakari Kiwelu, alisema tukio hilo limetokea usiku wa Novemba 6, mwaka huu, katika eneo la Mamba Kotela.

"Tumeamka asubuhi na kukuta hilo tukio, tulisikia kutokea kwa tukio hilo ambapo mwili wa Evarist ulikutwa pembezoni mwa barabara tayari amesha-poteza maisha. Wasamaria wema walimchukua na kuupeleka mwili huo katika hospitali ya Marangu," alisema Kiwelu.

Shuhuda mwingine, Rehema Mmochi alisema wanahisi chanzo cha tukio hilo ni wivu wa mapenzi au kisasi kwa kuwa baada ya tukio hilo watuhumiwa waliacha chombo walichokuwa wakitumia kama usafiri (bodaboda)

"Mpaka sasa hatujui sababu hasa ni nini lakini upo uwezekano ikiwa kisasi au wivu wa kimapenzi, tunasubiri polisi wamalize uchunguzi ili kutoa taarifa kamili,"alisema Rehema.

**MAJERUHI ANENA**

Eden Meela alisema walitoka nyumbani Marangu Kotela kuja Marangu Mtoni kwa ajili ya kutafuta chakula na njiani walikutana na mtu amesimamisha pikipiki isiyo na namba za usajili katikati ya barabara, ikawalazimu kusimama.

"Baada ya kusimama tu alichomoa panga kiunoni na kumkata kaka yangu aliyekuwa akiendesha pikipiki. Alimkata kwenye shingo na kisha kunishambulia na mimi ingawa nilimfahamu," alisema.



Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Balozi Liberat Mfumukeko akipokea hati ya utambulisho kutoka kwa Balozi wa Uingereza hapa nchini, David Wiliam Concar, katika makao makuu ya jumuiya hiyo, jijini Arusha jana. **PICHA: ASRAJI MVUNGI**

# Comoro yaipongeza Tanzania kufanya uchaguzi huru, haki

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Visiwa vya Comoro, Azali Assouman, ameipongeza Tanzania kwa kufanya uchaguzi huru, amani na haki.

Assouman alitoa pongezi hizo jana jijini Dar es Salaam alipokuwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa tayari kwa kuondoka nchini na kurejea Comoro baada ya kushuhudia uapisho wa Rais John Magufuli uliofanyika Novemba 5, jijini Dodoma.

Taarifa iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilisema Rais huyo aliielezea Tanzania kuwa ni nchi ya amani na utulivu wa kisiasa kwa kuwa wakati wote wa kuapishwa kwa Rais Magufuli aliona mambo ambayo yanapaswa kuigwa na mataifa mengine hususan nyakati za uchaguzi.

"Kwa kweli tangu nimefika hapa Tanzania nimeona mambo mazuri na ambayo tunapaswa kuyaiga sisi viongozi wa mataifa mengine," alisema Rais Assouman.

Mbali na kujifunza masuala mbalimbali yakiwamo ya uchaguzi, pia Rais Assouman aliahidi ushirikiano na serikali ya Tanzania katika nyanja mbalimbali zikiwamo diplomasia ya uchumi, biashara, uwekezaji na utalii.

"Najisikia niko nyumbani kwa sababu uhusiano wetu umeimarishwa zaidi. Uhusiano wetu umekuwa katika masuala ya kijamii, utamaduni, biashara na mambo mengine mengi," limebainisha Rais Assouman.

Balozi wa Tanzania nchini Comoro, Sylvester Mabumba, alisema serikali ya Tanzania itaendelea kushirikiana na Comoro katika kuhakikisha uchumi wa nchi zote mbili unakua zaidi.

"Sisi tuatendelea kushirikiana vyema na Comoro kibiashara ili kukuza sera ya 2025 tunaifikia ipasavyo kwa kuhakikisha kuwa uchumi wetu unafikia kiwango cha juu. Naamini kuwa tunapokuwa na masoko ya uhakika viswa vya Comoro, uchumi wetu utakuwa zaidi," alisema.

Naye Balozi wa Visiwa Vya Comoro nchini Tanzania, Dk. Ahmada El Badaoui Mohammed, alisema kuna fursa nyingi za kiuchumi ambazo Comoro na Tanzania zinaweza kushirikiana.

Rais Assouman aliwasili nchini Novemba 4, mwaka huu, kwa ajili ya kuhudhuria hafla ya uapisho wa Rais Magufuli uliofanyika Novemba 5, jijini Dodoma. Baada ya shughuli hiyo, alitembelea Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro na kujionea vivutio mbalimbali vya utalii nchini.

Serikali ya Tanzania na Visiwa Comoro zimekuwa zikishirikiana katika sekta mbalimbali zikiwamo, elimu, afya, biashara na uwekezaji.

## Aliyetoroka aongezewa kifungo jela

**Na Said Hamduni,** LINDI

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Lindi, imemhukumu kutumikia kifungo cha mwaka mmoja mkazi wa Ruangwa, Dunstan Kitenge (28) baada ya kupatikana na hatia ya kutoroka akiwa chini ya ulinzi wa vyombo vya dola.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi Elimo Massawe, baada ya kuridhishwa pasipo shaka na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, mshtakiwa alipewa nafasi ya kujitetea na kuiomba mahakama isimpe adhabu kali kwa madai alifanya hivyo kutokana na ugumu wa kuishi gerezani.

Baada ya utetezi huo, Mwanasheria wa Serikali, Abdulrhaman Mohamed, aliiomba mahakama kumpatia mshtakiwa adhabu kali kutokana na kitendo alichofanya cha kutoroka akiwa chini ya ulinzi, ili iwe fundisho kwake na wengine wenye tabia ya aina hiyo.

Mshtakiwa akiwa anatumikia kifungo gerezani, alitoroka akiwa chini ya ulinzi wa vyombo vya dola na baadaye kukamatwa akiwa amejificha kwenye kichaka.

Hakimu Massawe akitoa hukumu katika kesi hiyo namba 20/2020 kupitia kifungu 326 kifungu kidogo cha (1) Kanuni ya Adhabu sura ya 16 rejeo la 2002 kwa kuamuru kutumikia kifungo kingine cha miezi 12 jela.

Mwanzoni, ilidaiwa mahakamani hapo kuwa mshtakiwa alifanya utoro huo Januari 31, mwaka huu, akiwa chini ya ulinzi huku akiwa amefungwa pingu mikononi.

## Asasi yavitaka vyama kukubali ushindi wa JPM

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

SHIRIKA lisilo la Kiserikali la Mchomoro AIDS Combat Group (MACG) lililopo wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma, limevitaka vyama vya siasa kuukubali ushindi wa Rais John Magufuli.

Shirika hilo lilipewa kibali na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) cha kutoa elimu ya mpigakura katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo, Shazir Malamaye, alisema katika uchaguzi wowote ni lazima kuna kushinda na kushindwa, na kwasababu hiyo waliokuwa wanagombea wanatakiwa waelewe jambo hilo.

Malamaye alisema kwa mujibu wa takwimu za NEC, aliyekuwa mgombea wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Dk John Magufuli alipata kura 12,516,252 sawa na asilimia 84.4 ya kura zote zilizopigwa huku Tundu Lissu wa CHADEMA alipata kura 1,933,271 sawa na asilimia 13

Alisema kuwa siri kubwa ya ushindi wa CCM licha ya utendaji kazi wa Rais Magufuli katika awamu yake ya kwanza, ni kuwa kimejikita vijijini kuanzia ngazi ya mashina, matawi, wilaya, mkoa hadi taifa.

# Mkuu wa Wilaya Kahama aapa kumaliza mgogoro wachimbaji

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, amesema serikali imejipanga kumaliza mgogoro unaofukuta baina ya Ofisi ya Madini Mkoa wa Kahama na vikundi vya wachimbaji wa dhahabu katika machimbo ya Mwime, wilayani hapa.

Macha aliyasema hayo juzi wakati akijibu maswali ya waandishi wa habari waliotaka ufafanuzi juu ya mgogoro unaohusisha wachimbaji hao wanaoituhumu ofisi ya madini kuomba rushwa ya Sh. milioni tano kila wiki ili wakabidhiwe eneo jipya.

Katika maelezo yake, Macha alisema hakuna vurugu yoyote katika mgodi huo isipokuwa kuna hali ya kutoelewana baina ya vikundi hivyo katika eneo linaloonekana kuwa na dhahabu.

"Ni kweli nililetewa taarifa za mgogoro lakini sijashuhudia. Kwa mujibu wa mwongozo kutoka sekta ya Madini, kijieneo kinachofumuka dhahabu lazima kitengenezewe utaratibu wa kuweka msimamizi atakayekusanya kodi za serikali na tunataka vikundi vya maeneo yale yale na kama hajapatikana mtu wao lazima malalamiko yatokee," alisema.

Awali, Mwenyekiti wa Kikundi cha Isalenge Iyenze Gold Mine, Tabu John, alisema kikundi chake hakihusiki kwa kuwa ndicho kilichoshinda kupewa hati ya usimamizi wa eneo hilo ili kukusanya mapato ya serikali na kusimamia wachimbaji wengine.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Mwime 2 Gold Mine, Ali Masele, akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, alisema kikundi chao kimekuwa na tatizo la kuvamiwa mara kwa mara na kikundi cha Kabela Gold Mine ambacho ni mwavuli wa Isalenge Iyenze.

Alibainisha kuwa eneo wanalogombania liko mpakani mwa leseni zao nne jambo ambalo linawashangaza wanakikundi hao kwamba ofisi ya madini wanakabidhi eneo hilo kwa watu ambao wako mbali na hawajapatafiti.

Masele aliongeza kuwa kikundi chake, tangu kimeanza uzalishaji hadi sasa, kimetoa zaidi ya Sh. milioni 360 kwa kipindi cha miezi mitatu sambamba na kuchangia huduma za kijamii kama elimu, afya, maji na miundombinu bora ya barabara kwa wananchi wa Mwime.

"Kwa kweli tunaiomba serikali iingilie kati mgogoro wetu. Hatukubali kwa kuwa tumeshawekeza gharama zetu na hao walioonekana kutoa rushwa ili walitwae eneo hilo hawajafanya lolote," alisema.

Katibu Mtendaji wa Mgodi wa Mwime 2 Gold Mine, Justine Misalaba, alisema mwezi mmoja uliopita, maofisa wa madini waliwafuata na kuwaomba waingie nao ubia kwenye eneo lililoko mbele yao linalotarajiwa kutangazwa kuwa 'Rush' (eneo jipya lenye madini).

# Serengeti yashinda tuzo hifadhi bora

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

HIFADHI ya Taifa Serengeti, imeshinda tuzo ya kimataifa na kutangazwa kuwa hifadhi bora katika Bara la Afrika kwa mwaka huu.

Hayo yalisemwa jana kupitia taarifa ya Kamishna Msaidizi Mwandamizi Mawasiliano wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Paschal Shelutete, iliyotolewa kwenye mitandao ya kijamii.

Shelutete alisema tuzo hizo zilitangazwa Novemba 9, mwaka huu, na Taasisi ya World Travel Awards (WTA) ya nchini Marekani kwa njia ya mtandao.

"Hii ni mara ya pili kwa hifadhi ya Taifa Serengeti kushinda katika kundi la hifadhi zinazoongoza kwa ubora zaidi bara la Afrika baada ya kushinda pia mwaka jana 2019," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Serengeti imeibuka na ushindi katika shindano hilo lililoshindanisha hifadhi zingine za Central Kalahari (Botswana), Etosha (Namibia), Kidepo Valley (Uganda), Kruger (Afrika Kusini) na Maasai Mara National Reserve (Kenya).

"Serengeti inajivunia umaarufu wa msafara wa nyumbu wahamao zaidi ya milioni 1.5, aina mbalimbali za wanyamapori wanaopatikana kwa wingi, mandhari nzuri ya kuvutia pamoja na shughuli mbalimbali za utalii zinazovutia watalii wengi," ilisema taarifa hiyo.

Kutokana na ushindi huo, TANAPA imewashukuru Watanzania, serikali na wadau wa utalii waliotumia muda wao kupiga kura na kufanya Serengeti kuwa mshindi wa hifadhi bora zaidi kwa Bara la Afrika kwa mwaka huu.

**Hii ni mara ya pili kwa hifadhi ya Taifa Serengeti kushinda katika kundi la hifadhi zinazoongoza kwa ubora zaidi bara la Afrika baada ya kushinda pia mwaka jana 2019.**



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanaosubiri kuteuliwa wasitarajie mteremko

**BAADA** ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu, Rais John Magufuli ameanza mchakato wa kuunda serikali yake katika ngazi mbalimbali za uteuzi.

Tayari Rais Magufuli ameshaanza kutekeleza jukumu hilo la kikatiba kwa kumteua na kumwapisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Prof. Adelardus Kilangi. Baadaye atamteua waziri mkuu, mawaziri, makatibu wakuu, wakuu wa mikoa, wilaya, makatibu tawala wa mikoa na wilaya na nafasi zingine. Ikumbukwe kuwa Rais pia amepewa mamlaka kikatiba kuteua wabunge 10.

Kipindi hiki, kuna watu kadhaa wanafikiria nafasi za kuteuliwa, wakiamini kuwa kuna mambo mazuri wameyafanya, hivyo asante kwao ni kuteuliwa.

Uzoefu umeonyesha kwamba kuna watu ambo hushiriki kwenye mchakato wa kampeni za Chama Cha Mapinduzi (CCM), na baada ya uchaguzi kujipa matumaini kwamba watakumbukwa kwa kupewa nafasi za kuteuliwa.

Aidha, wapo watu wengine ambao wamekuwa wakisubiri kukumbukwa kwa kuteuliwa tangu kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, hivyo nao hawajakata tamaa na wanaendelea kusubiria.

Kadhalika, kuna wanaoendelea kushika nafasi hizo tangu mwaka 2015 pamoja na waliopata uteuzi baada ya hapo. Wote hawa wanasubiria kusikia kama itampendeza rais na kuwabakisha.

Kimsingi, kwa wanaoendelea na nafasi za kuteuliwa, wengi wao wanahofia mabadiliko ya serikali, ambayo Rais Magufuli atayafanya siku chache zijazo. Rais Magufuli pia aliligusia suala hilo juzi katika hafla ya kumwapisha Prof. Kilangi, kwa kueleza kuwa kigezo cha kuteuliwa ni utendaji mzuri na wenye tija na ufanisi.

Alisema kwenye Baraza lake la Mawaziri kuna mawaziri watabaki na baadhi wataachwa, huku akisisitiza kuwa kigezo kikuu ni utendaji wa mteuliwa na si vinginevyo.

Hata hivyo, alieleza kushangazwa na baadhi ya wateule wake kuingiwa na hofu wakati akijiandaa kufanya uteuzi, huku akiwataja wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya na wakurugenzi.

Sisi tunaona kuwa hakuna sababu za wateule wake kuingiwa na hofu ya kutokuteuliwa, isipokuwa wajipime wenyewe kwanza kama wamefanya mambo mazuri. Haiingii akilini kumuona kiongozi au mtendaji ambaye ameshindwa kutimiza majukumu yake akiwa na matarajio ya kurejeshwa kwenye nafasi yake.

Rais Magufuli wakati wa kampeni takribani zaidi ya miezi miwili amepita maeneo yote ya Tanzania na kuona ni wapi wateule wake wamefanya vizuri na kukidhi matarajio ya Watanzania wengi. Pia ameona maeneo ambayo wateule wake wamefeli kutekeleza majukumu yake.


Kwa waliotekeleza vizuri majukumu yao bila shaka hatakuwa tayari kuwaacha, lakini kwa waliofeli ni dhahiri atawaweka kando na kuingiza atakaowaona wanaweza kuthubutu. Kuna mambo mengine mawili ambayo yatamfanya ayazingatie katika kufanya uteuzi wake. Mosi, ni ilani ya uchaguzi ya CCM ambayo aliinadi kwa wananchi wakati wa kampeni, ambayo imesheheni ahadi lukuki za mambo ya kutekeleza.

Ili kufanikisha utekelezaji wake unafanikiwa, ni dhahiri atahakikisha anawateua watu ambao ni waadilifu, makini, wachapa kazi na wanaojituma.

Pili, Rais Magufuli wakati wa kampeni alisikia baadhi ya mambo ya kuikosoa serikali yake kutoka upande wa upinzani, hivyo atahakikisha anaunda timu ya wateule wenye uthubutu wa kuyapatia ufumbuzi.

Tunawashauri wanaosubiri uteuzi bila kufanya mambo yenye tija na ufanisi wasitegemee mteremko, utendaji wao ndio utakaoamua uteuzi wao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Christina Mwakangale

## Muungwana Lazima Nilonge

# Vyombo vya uchaguzi visipuuze, vijisafishe

**UCHAGUZI** wa mwaka huu umekamilika na baadhi ya asasi zilizoutazama zimewasilisha ripoti na mapendekezo kwa vyombo vya kuratibu mchakato huo, kuhusu namna bora ya kuuboresha kwa siku zijazo.

Ripoti inayotolewa hivi karibu na asasi ya Kituo cha Sera cha Kimataifa (CIP) Afrika, kuhusu uchaguzi huo, inabaini masuala kadhaa yakiwamo mafanikio na matatizo ya zoezi hilo la kidemokrasia ambalo kwa Tanzania lilifanyika Oktoba 28.

Mkurugenzi Mtendaji wa CIP, Omar Mjenga, anasema uchaguzi wa mwaka huu umefanikiwa na kwamba idadi ndogo ya wapigakura milioni 14.8 sawa na asilimia 50 ya waliojiandikisha kwenye daftari la wapigajikura ndiyo iliyojitokeza.

Anasema watazamaji wake takribani 100 waliokuwa kwenye mikoa 17 ikiwamo Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kilimanjaro, Kigoma, Mara, Mbeya, Mtwara, Mwanza, Lindi, Rukwa, Ruvuma, Tabora, Tanga, Pemba na Zanzibar wana mambo muhimu ya kushauri.

Anasema siku ya upigaji kura vituo vya kupigia kura vilifunguliwa kwa wakati na vifaa licha ya baadhi kucheleweshwa kutokana na matatizo ya usafiri na maeneo mengi hayafikiki kwa urahisi.

Mjenga anasema usalama uliimarishwa, lakini wananchi walidai kwamba, uwepo wa maofisa wengi wa usalama uliwaogopesha wapigakura wengi na inaweza kuwa sababu ya kutojitokeza.

Pia anabainisha kwamba baadhi ya wasimamizi wa vituo vya uchaguzi hawakuwa na elimu ya kutosha kuhusu majukumu yao.

Aidha, baadhi ya vituo vilikosa karatasi za kura na masanduku ya kura kucheleweshwa hasa ya urais.

"Katika maeneo mengine kama Rukwa, wapigakura wengine walishindwa kufuatilia majina yao kwenye orodha ya wapigakura na hawakusaidiwa vya kutosha na maofisa waliokuwa wakisimamia uchaguzi," anasema Mjenga.

> **Kwa kuwa kulikuwa na watazamaji wengi, CIP inapendekeza kwamba NEC na ZEC ziitishe watazamaji wote waliothibitishwa kukutana na kushirikishana yale yaliyotokea wakati wa uchaguzi kwa uboreshaji zaidi wa mchakato ujao.**

Anasema Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Tume ya Uchaguzi Zanzibar ZEC zishughulikie malalamiko yaliyoripotiwa kuhusu usimamizi wa mchakato, ili uchaguzi ujao uwe wa mafanikio ikiwamo kuwa na idadi inayoridhisha ya wapigakura.

Anasema CIP ilibaini kuwa moja ya kituo kilichoandikisha wapigakura 450, hadi saa 10 jioni, kilikuwa hakijapokea robo ya idadi hiyo.

Anasema katika vituo vingi mawakala wa vyama walikuwa wanatoka CHADEMA, CCM na ACT-Wazalendo na kwamba vingine vilikumbwa na ucheleweshaji wa kuruhusu mawakala wa vyama kutekeleza majukumu yao.

Aidha, katika uchaguzi huu CIP imeripoti uwapo wa idadi kubwa ya wanawake wapigakura ikilinganishwa na wanaume.

Anasema CIP inapendekeza kunufaika utafiti, sababu ya kuwapo kwa idadi ndogo ya wapigakura katika uchaguzi mkuu mwaka huu, pamoja na mwamko mkubwa wa kisiasa uliokuwapo.

"Pia, baadhi ya maofisa wa uchaguzi hawakujua sheria na taratibu zinazosimamia uchaguzi, hivyo tunapendekeza kuajiri maofisa wenye sifa na mpango bora wa mafunzo kwa maofisa wa uchaguzi."

"Kwa kuwa kulikuwa na watazamaji wengi, CIP inapendekeza kwamba NEC na ZEC ziitishe watazamaji wote waliothibitishwa kukutana na kushirikishana yale yaliyotokea wakati wa uchaguzi kwa uboreshaji zaidi wa mchakato ujao," anasema Mjenga.

Tanzania Bara ilkuwa na vituo vya kupigia kura 80,155 wakati Zanzibar walikuwapo wapigakura 566,352 ambao walijiandikisha kupiga kura pamoja na vituo 1,413.

HABARI KITAIFA

# DC aona fursa stendi mpya

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MKUU wa Wilaya ya Morogoro, Bakari Msulwa, ameushauri uongozi wa Manispaa ya Morogoro kutumia mbinu mbadala za kuwavutia madereva na wananchi kuiwezesha stendi ya kisasa ya daladala ya Mafiga iliyojengwa kwa fedha nyingi, kusaidia kukuza uchumi.

Msulwa aliyasema hayo jana alipozindua mradi wa stendi ya daladala ya Kaloleni iliyoko Kata ya Mji Mpya, Manispaa ya Morogoro iliyojengwa kwa Sh. milioni 644 za mkopo wa Benki ya Dunia chini ya fedha za uboreshaji Miji (ULGSP).

Mradi huo uliofadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia ULGSP, umetekelezwa na mkandarasi M/s Nandhra Engineering and Construction Co Ltd wa Morogoro.

Manispaa ya Morogoro ilikuwa inatekeleza miradi miwili tofauti ya stendi za daladala ambapo kwa mradi wa ujenzi wa stendi ya Mafiga, imetumia Sh. bilioni 5.2.

Kwa Stendi ya Mafiga ambayo bado haijafunguliwa, mkuu huyo wa wilaya aliutaka uongozi wa manispaa kuanzisha gulio la Jumamosi na Jumapili na kutengeneza mabanda ya kufanyia biashara ili kuwapo na shughuli za kiuchumi ambazo ni kichocheo cha madereva na wamiliki wa daladala kuitumia ipasavyo stendi hiyo.

Alisema manispaa hiyo ikichukua na hadhi ya jiji, eneo hilo la Stendi ya Mafiga halitakuwa tena nje ya mji, hivyo kuwataka wananchi na madereva kujiandaa kisaikolojia.

Alisema hivi sasa watu wameongezeka, magari yameongezeka zikiwamo pia bajaji na pikipiki, hivyo haiwezekani kuendelea kuwa na manispaa ambayo watu wanaendelea kusongamana kana kwamba sehemu nyingine za kufanya shughuli za uchumi zimekwisha.

Msulwa alisema kuwa akiwa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, alishatoa maelekezo kwa uongozi wa manispaa hiyo kutosifirikia kabisa kufanyika kwa operesheni ya nguvu, bali ni operesheni ya akili ya kuwashirikisha wananchi watoke maoni yao kufanikisha kusisimua uchumi wao eneo la Stendi ya Mafiga.

Alisema viongozi wa manispaa wakutane na viongozi wa daladala ili kujadiliana na kufikia mwafaka wa kutatua shida zilizojitokeza huku akizitaka mamlaka zote zinazosimamia usafirishaji wa abiria, kukutana na kuangalia njia zinakuwa na uwiano na kukidhi mahitaji ya sasa.

Stendi hiyo ya kisasa ya daladala ina uwezo wa kuchukua magari 150 kwa wakati mmoja, eneo la maegesho ya taksi 40, bajaji 32 na bodaboda 23.

**Manispaa hiyo ikichukua na hadhi ya jiji, eneo hilo la Stendi ya Mafiga halitakuwa tena nje ya mji, hivyo kuwataka wananchi na madereva kujiandaa kisaikolojia.**

# Polisi Dar wafunga barabara kisa mvua

**Na Christina Mwakangale**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limelazimika kuzifunga kwa muda baadhi ya barabara hususan zinakokatiza Mto Msimbazi, kutokana na mvua kubwa inayoendelea kunyesha.

Barabara zilizofungwa ni pamoja na ile ya Morogoro ambayo mara nyingi kipindi cha mvua imekuwa ikifungwa katika kipande chake kinachokatiza eneo la Jangwani.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), ilitoa tarifa ya kuwapo kwa mvua kwa siku tano mfululizo kuanzia Jumapili kwa mikoa ya Tanga, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam na visiwa vya Zanzibar na Mafia.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, aliiambia Nipashe jana kwamba pamoja na mvua hiyo kutoleta madhara ya moja kwa moja kwa binadamu, jeshi hilo limechukua tahadhari kwa kufunga barabara ambazo mito hufurika.

'Tumefunga njia, Jangwani, Kigogo kuna wakati tulifunga wakati maji yalipokuwa mengi ili kudbiti watu wasiende, wabaki salama.

"Hatujapata madhara yoyote, hakuna madhara kwa maisha ya binadamu. Njia mbadala ni Bagamoyo, Pugu, kwa ambao wanatoka nje ya mji na njia zote ambazo hazina vikwazo. Vikwazo ni Jangwani na Kigogo.

Alisema jeshi hilo linatoa tahadhari kwa wananchi hasa wanaoishi kwenye mabonde ili kuepuka mafuriko.

Alisema walezi na wazazi pia wawaangalie watoto wao na kutowaacha wakizunguka kwenda maeneo tofauti bila uangalizi maalum.

Taarifa ya Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Agnes Kijazi, ilisema mvua hiyo italeta madhara kwa baadhi ya maeneo kutuama maji.

"Kwa kiasi kikubwa mvua hii itasababisha kutuama kwa maji maeneo ya makazi ya watu, lakini inaweza ikaleta athari ya miundombinu," alisema Dk. Kijazi kwenye taarifa hiyo.

Pia, aliwataka wananchi kuchukua tahadhari na kusafisha mitaro ili kurahisisha upitaji wa maji.



Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi, akizungumza katika kongamano la pili la wataalamu wa sayansi ya magonjwa yasiyoambukiza, lilioandaliwa na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Tembo waua watu watatu, kujeruhi

**Na Stevie Chindiye ,** TUNDURU

WATU watatu wakazi wa vijiji vya Mtonya, Kata ya Mindu na Tulieni Kata ya Nakapanya wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, wamekufa kwa kukanyagwa na tembo.

Tukio hilo lilitokea baada ya wanyama hao kuvamia kwenye maeneo ya vijiji vyao.

Aidha katika tukio hilo, mkazi wa Kijiji cha Mtonya Zuberi Wakati Mchopa (70), amelazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Tunduru baada ya kujeruhiwa vibaya na wanyama hao.

Ofisa wanayamapori wa Wilaya ya Tunduru, Limbega Hassan Ally, alisema matukio hayo yalitokea kwa nyakati tofauti Novemba 9, mwaka huu na kwamba baada ya kupokea taarifa hizo ameshapeleka askari wenye silaha kwa ajili ya kuwafukuza tembo hao ili wasiendelee kuleta madhara kwa wananchi.

Limbega aliwataja waliofariki ni Jamira Mathayo Mchopa (47), Muslimu, Mmakua mkazi wa Kijiji cha Tulieni Kata ya Nakapanya wilayani humo, ambaye alishambuliwa na wanyama hao majira ya saa 10:00 asubuhi akiwa shambani kwake.

Limbega alimtaja mtu mwingine aliyefariki ni Jastini Gideon Mchopa (54) Muslimu, mkazi wa kijiji cha Mtonya Kata ya Mindu ambaye alishambuliwa majira saa 09:30 akiwa shambani.

Kwamujibu wa Limbega, mtu mwingine aliyepoteza maisha ni Stephano Hassan Joseph (78), mkazi wa Kijiji cha Mtonya Kata Mindu, ambaye alishambuliwa na wanyama hao akiwa shambani majira ya saa 08:00 asubuhi.

Alisema chanzo cha matukio hayo ni wanachi wengi katika maeneo ya Wilaya ya Tunduru kulima katika njia za tembo (shoroba) kutoka kwenye hifadhi za Lumesule inayopita wilayani Nanyumbu Mkoani Mtwara, Mwambesi na Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere (Selous) maeneo ambayo wanyama hao hupita kuelezea Hifadhi ya Niasa iliyopo Msumbiji.

Madiwani wateule wa kata za Mindu, Nakoko Richard Bazil na Abdul Machaura wa Kata ya Nakapanya, walisema kuwa kwa sasa wanyama hao ni wengi na wanatishia usalama wa wananchi ikiwamo kuharibu mazao yao.

Limbega aliwataka wananchi wa maeneo ambayo yamekuwa yakisumbuliwa na wanyama waharibifu wa mazao wakiwamo tembo kutembea kwa makundi kila wanapo kuwa wanaenda mashambani ili kusaidiana inapotokea wanyama hao kuvamia maeneo yao.

# Shirika kuanzisha chuo cha ufundi

**Na Christina Haule,** MOROGORO

SHIRIKA linalojihusisha na kutoa elimu kwa vijana na masuala ya Ukimwi (Faraja Trust Fund), limeazimia kuanzisha chuo cha ufundi kisicho rasmi ili kusaidia watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu kujikimu kimaisha.

Mkurugenzi Mtendaji wa Faraja, Dk. Lucy Nkya, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, mjini hapa.

Alisema kuanzishwa chuo hicho katika majengo ya mojawapo ya shule za watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu kilichopo kata ya Kingo, kutasaidia vijana kupata elimu zaidi.

Dk. Nkya alisema ameanza kumiliki vituo viwili vya kutoa elimu ya msingi vilivyoko kata za Kingo na Chamwino kwa watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu na wa mitaani tangu mwaka 1998 lakini baada ya masomo, wengi wao wamekuwa wakibaki mitaani.

Alisema kuanzishwa kwa chuo hicho kisicho rasmi mkoani hapa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (VETA) Kanda ya Mashariki chini ya Mradi wa Ujana ni Mtaji ulioanzishwa mwaka 2019, kutasaidia watoto hao kujifunza kazi rahisi za mikono, hivyo kujishughulisha na kuendesha maisha yao.

"Wako vijana wengi ambao wamemaliza kwenye vituo hivyo viwili wamepata nafasi za kuwa wahandisi, walimu na wafanyabiashara baada ya kupata misaada. Lakini wale waliokosa kuendelezwa wamekuwa hawana la kufanya, wameamua kurudi mitaani na wengine kujiingiza kwenye magenge ya kihuni," alisema Dk. Nkya.

Alisema katika chuo hicho, vijana wenye umri wa kuanzia miaka 14 watapata elimu ya mambo mbalimbali ikiwamo mama na baba lishe, saluni, ushonaji, useremala, kilimo na ujenzi jambo ambalo pia litasaidia kupunguza vitendo vya uhalifu mkoani hapa.

Pia aslisema kwa kushirikiana na VETA na baadhi ya watu waliowapa elimu ya ujasiriamali wakati wakisaidia watoto walio katika mazingira magumu kielimu mwaka 1998, wanaweza kuwaelimisha darasani na baadaye kwa vitendo, hivyo kijikimu kimaisha.

Alisema watoto wengi waliowapokea kwenye vituo vya kusomesha watoto wa mazingira magumu wametokana na wazazi wao kufariki dunia kwa janga la UKIMWI, wazazi kutengana na migongano mbalimbali ya kifamilia.

Naye mwalimu wa shule ya watoto wanaotoka kwenye mazingira magumu iliyoko chini ya Faraja, Nora Makuga, alisema wamekuwa wakipokea watoto wanaoanza elimu ya msingi wakiwa na umri mkubwa hata miaka 14 hadi 15 jambo ambalo si sahihi kwa kituo hicho.

Alisema kimsingi watoto wanaostahili kuingia shuleni kwa walioikosa ni wale wa miaka 9-11 ili wafanya mtihani wa darasa la nne na kuendelea na elimu na wakifaulu vizuri kufanya mtihani wa darasa saba.




Mkuu wa Mauzo na Usambazaji wa Vodacom Tanzania Plc, George Lugata (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa huduma mpya ya mkopo wa simujanja itakayowezesha wateja wake kukopeshwa simu katika maduka ya kampuni hiyo nchini. Kulia ni Meneja Mkuu wa Laina Finance Ltd ambao ni wabia wa huduma hiyo, Mrisho Shomari. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vikundi ujasiriamali vyatakiwa kujisajili

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKURUGENZI wa asasi isiyo ya kiserikali ya Wakala wa Maendeleo Mkoa wa Pwani (DPA), Rachel Jacob, amevitaka vikundi vya wajasiriamali kujisajili kisheria ili kunufaika na mikopo.

Jacob aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari huku akisisitiza kuwa hatua ya vikundi hivyo kujisajili itaviwezesha kupata mikopo inayotolewa kwenye halmashauri na taasisi za kifedha.

Alisema kazi ya asasi yao ni kutoa elimu ya uraia ikiwa ni pamoja na ujasiriamali na kuhamasisha wananchi kushiriki kwenye mikutano ya kijamii kuanzia ngazi ya serikali ya mtaa.

Pia alisema wamekuwa wakiwasaidia wanavikundi kuandaa katiba, mihutasari na mipango yao ya kuomba fedha na kwamba baadhi ya vikundi tayari vimejisajili na kupata fedha.

Alisema wanaendelea kuihamasisha jamii kuwa na vikundi vya ujasiriamali ili kukabiliana na hali ngumu ya kimaisha na kuwahimiza wasajiliwe ili kufikia malengo yao.

Jacob pia alisema mbali ya kuhamasisha jamii kusajili vikundi pia wamekuwa wakiwaunganisha na wadau wengine ambao wanahusika na uboreshaji wa utengenezaji bidhaa likiwamo Shirika la Maendeleo la Viwanda Vidogo (SIDO).

Mkurugenzi huyo alisema asasi zisizo za kiserikali zina mchango mkubwa katika suala la maendeleo na kwamba hadi kufikia Septemba mwaka huu wametoa elimu kwa watu 134 katika Wilaya ya Kibaha.

**Kazi ya asasi yao ni kutoa elimu ya uraia ikiwa ni pamoja na ujasiriamali na kuhamasisha wananchi kushiriki kwenye mikutano ya kijamii kuanzia ngazi ya serikali ya mtaa.**

# 'Serikali iingilie mgogoro wa ardhi'

**Na Frank kaundula,** MOROGORO

WANANCHI wa Kijiji cha Doma wilayani Mvomero mkoani Morogoro, wameiomba serikali kuingilia kati mgogoro wa mpaka baina yao na Hifadhi ya Taifa Mikumi uliodumu kwa muda mrefu.

Wakizungumza katika mkutano ulioitishwa na Mkuu wa Wilaya ya Mvomero na kuwakutanisha wakazi wa kijiji hicho na uongozi wa Hifadhi ya Taifa Mikumi, baadhi ya wakazi wa kijiji hicho akiwamo Fikiri Maumba, walisema hatua ya kuwekwa mipaka bila kushirikishwa ni kwenda kinyume cha sheria.

Maumba alisema kuwa baada ya maofisa wa hifadhi kuweka jiwe mpakani, kumesababisha wananchi kukosa maeneo kwa ajili ya shughuli zao za kilimo huku akidai kufanyiwa vitendo vya unyanyasaji kwa wakazi wanaoingia katika eneo hilo.

"Wamekuja kijijini na kupanda jiwe la mpaka bila wahusika kushirikishwa na tulivyowauliza wakadai eneo ni lao, lakini siyo kweli, lakini pia hata wananchi wakijaribu kuingia kutafuta hata kuni wanaishia kupigwa na kunyanyaswa," alisema.

Mtendaji wa Kijiji hicho, Lightness Njovu, alisema kiini cha mgogoro ni baada ya viongozi wa hifadhi kuweka alama za mipaka maeneo yanayodaiwa kumilikiwa na kijiji.

"Ni kweli mgogoro huu upo na ulianza baada ya hifadhi kuweka mipaka bila kushirikisha viongozi wa kijiji, mbali na kukwamisha shughuli za maendeleo, upangaji wa matumizi bora ya ardhi kijijini lilikwama na hatujui tutafanyaje ndiyo maana tunaomba msaada serikalini," alisema.

Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Mikumi, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Mathew Mombo, alisema maeneo ya hifadhi yanaendeshwa kwa misingi ya kisheria na kwamba baadhi ya viongozi walishirikishwa katika mchakato huo.

Alisema kuwa pamoja na mambo mengine, mgogoro huo ameukuta hivyo atahakikisha anaufuatilia kiundani ili kujiridhisha juu ya hatua zilizochukuliwa wakati huo na kuahidi kushirikisha pande zote ikiwamo viongozi wa kijiji katika kujua ukweli.

"Sisi ni taasisi ya serikali, haturuhusiwi kuchukua ardhi ya wananchi kwa matakwa yetu, lazima mipaka yetu ipite kwenye maeneo yaliyoainishwa. Kwa hiyo, tutarudi tena tutawaita wale wahusika na kuwashirikisha viongozi wa vijiji kuhakikisha yale yaliyofanyika tunayaweka sawa," alisema Kamishna Mombo.

Akitolea ufafanuzi mgogoro huo, Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Albinius Mgonya, alisema msimamo wa serikali ni kumalizika kwa mgogoro huo na kutoa fursa kwa kila mmoja kuendelea na shughuli za uzalishaji.

Aliwatoa wasiwasi wananchi kuwa tayari serikali imeanza kushughulikia migogoro yote ya ardhi ndani ya wilaya hiyo ikiwamo kuweka usimamizi mzuri katika mashambapori ambayo hayajaendelezwa.

"Serikali tumeshakaa na maeneo yote yenye mgogoro tumeshaainisha na baada ya muda mfupi, yanamalizika. Kwa hiyo, wananchi wa Doma muwe watulivu," aliahidi.

# Angalizo kula matunda bila ya kunawa mikono

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAKAZI mkoani Shinyanga, wametahadharishwa kuacha tabia ya kula matunda ovyo bila ya kunawa mikono wala kuyaosha, hasa katika msimu huu wa maembe ili kuepuka kupatwa na magonjwa ya mlipuko.

Ofisa Afya Mkoa wa Shinyanga, Neema Simba, alisema hayo juzi wakati akizungumza na vyombo vya habari, kuwa katika msimu huu wa matunda hususani embe, wananchi wanapaswa kuwa makini kuzingatia usafi wa unawaji mikono na kuosha matunda hayo, ili kujikinga na magonjwa ya mlipuko.

Alisema kuna baadhi ya watu wamezoea kula matunda bila ya kunawa mikono wala kuyaosha, kitendo ambacho ni hatari wa afya zao, ikiwamo kupatwa na magonjwa ya mlipuko yatokanayo na kula uchafu.

"Kipindi hiki ni msimu wa matunda aina ya embe, nawaomba sana wananchi wazingatie suala la usafi kwa kunawa mikono na kuosha matunda hayo kabla ya kula, ili kuepuka kupatwa na magonjwa ya mlipuko kikiwamo kipindupindu au kuhara, " alisema Simba.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Yudas Ndungile, aliwataka pia wafanyabiashara ambao wanauza matunda hayo wazingatie usafi katika biashara zao, hasa kipindi hiki cha mvua ambacho huibuka magonjwa mengi ya mlipuko.

Mmoja wa wakazi wa mkoa huo, Ester Lucas, alisema inapaswa kutolewa elimu kwa wananchi kuacha kula matunda bila ya kunawa mikono wala kuyaosha, hasa katika maeneo ya vijijini.

**Kipindi hiki ni msimu wa matunda aina ya embe, nawaomba sana wananchi wazingatie suala la usafi kwa kunawa mikono na kuosha matunda hayo kabla ya kula, ili kuepuka kupatwa na magonjwa ya mlipuko kikiwamo kipindupindu au kuhara.**

# Magunia yalivyokwamisha korosho kuingia mnadani

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

UHABA wa magunia kwa wakulima wa korosho wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wilayani Masasi na Nanyumhu (MAMCU), umesababisha mamia ya tani za korosho kushindwa kuingia kwenye minada ya mauzo kutokana na wakulima wengi kukosa magunia ya kuhifadhia kwa zaidi ya mwezi mmoja sasa.

Hayo yalielezwa jana wilayani Masasi mkoani Lindi na baadhi ya wakulima wa korosho wa vyama mbalimbali vya msingi (AMCOS) vya wilaya hizo walipokuwa wakizungumza na gazeti hili kuhusu mwenendo wa minada ya korosho.

Walisema kwa zaidi ya mwezi mmoja sasa kumekuwapo na tatizo kubwa na sugu la ukosefu wa magunia katika chama chao, hivyo wakulima wengi wa korosho zao zimekwama kupelekwa katika minada kwa ajili ya kuuzwa.

Peter Jamali kutoka Mpeta AMCOS wilayani Masasi, alisema hali ya korosho za wakulima kwenye vyama vya msingi ni mbaya kwa kuwa nyingi zimehifadhia kwenye viroba ambavyo havina sifa ya kuihifadhia.

Alisema korosho zingine zimewekwa sakafuni kutokana na uhaba wa magunia kutoka kwenye chama kikuu kwenda katika vyama vya msingi.

**Vyama vyetu vya msingi viko katika hali mbaya sana...korosho zetu zinashindwa kwenda mnadani kutokana na uhaba wa magunia tunaomba tupatiwe magunia ya kutosha.**

"Vyama vyetu vya msingi viko katika hali mbaya sana...korosho zetu zinashindwa kwenda mnadani kutokana na uhaba wa magunia tunaomba tupatiwe magunia ya kutosha," alisema Jamali.

Jamali alisema kutokana na hali hiyo, kuna uwezekano mkubwa wa korosho hizo kupoteza ubora wake, na kuwa zitakapokuwa zinaingia kwenye mnada zitakosa ubora na kupelekea kuuza kwa bei ndogo.

Alisema ni vigumu kufahamu ni kiasi gani cha tani za korosho kwa sasa ambazo zinashindwa kwenda kwenye maghala makuu kwa ajili ya kuingia kwenye minada.

Mkulima aliyejitambulisha kwa jina la Ajuwaye wa Wilaya ya Nanyumbu, alisema wanashangazwa kuona katika MAMCU hakuna magunia miezi miwili sasa, hali ambayo inasababisha korosho nyingi kukaa bila ya kwenda kwenye minada, hivyo wanaomba serikali zifanye jitihada za kuwakomboa wakulima hao.

Salumu Mwarabu, Katibu wa Mpemwena AMCOS, alisema kuwa korosho zinakwenda katika minada, lakini ni kidogo ukilinganisha na tani za korosho za wakulima ambazo zinashindwa kuuzwa kutokana na kukosa magunia.

Meneja wa MAMCU tawi la Wilaya za Masasi na Nanyumbu, Joseph Mmole, alikiri kuwapo tatizo la uhaba wa magunia, na kwamba linasababishwa na wakala ambaye alipewa kusambaza magunia kushindwa kusambaza vifungashio hivyo kwa wakati.

"Ni kweli kuna tani nyingi za korosho za wakulima zimekwama kuingia katika minada iliyopita kwa ajili ya wakulima kukosa magunia ya kuhifadhia korosho zao, lakini tunaendelea kufuatilia ili gunia hizo ziweze kupatikana za kutosha na wakulima waweze kuweka mazao yao kwa ajili ya kupeleka mnadani," alisema Mmole.

Mmole alisema mahitaji ya magunia kwa Chama Kikuu cha MAMCU tawi la Masasi na Nanyumbu ni jumla ya magunia milioni moja, lakini mpaka sasa gunia zilizopatikana na kutumika ni 500,000 pekee, hivyo kufanya kuwapo kwa uhaba mkubwa wa magunia ndani ya MAMCU.



Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Sipora Liana (wa pili kushoto), akionyesha maendeleo ya ujenzi wa kituo cha mabasi ya mikoani na nchi jirani cha Mbezi Luis, jijini humo mwishoni mwa wiki, ambao umefikia asilimia ya 90. Kushoto ni msimamizi wa mradi huo kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi, Dk. Godwin Maro. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbinu kukabiliana na kisukari zaanikwa

**Na Christina Mwakangale**

JAMII imeshauriwa kubadili mtindo wa maisha kwa kuzingatia lishe bora, ili kukabiliana na ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza hususan kisukari.

Bingwa wa Magonjwa ya Homoni kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Wolfgang Bernard, alisema ugonjwa wa kisukari unaendelea kuwa tatizo kubwa duniani.

Dk. Bernard aliyasema hayo jana, ili kukuza elimu kwa umma kuelekea Siku ya Kisukari Duniani, inayoadhimishwa Novemba 11, kila mwaka.

"Kisukari ni tatizo kubwa sana duniani na tatizo linaongezeka kila mwaka duniani," alisema bingwa huyo.

Aidha, kati ya sababu za ugonjwa huo, ambazo kwa kipindi tofauti huzitaja Dk. Bernard, alisema ulaji wa vyakula vya wanga na vyenye sukari zaidi husababisha mwili kuongezeka uzito na kuweka akiba mwilini.

"Vyakula vya wanga kwa wanaofanya kazi ngumu inaweza isiwe tatizo, kama vile wabeba zege, tofauti na waofanya kazi maofisini ambao hukaa muda mrefu bila kuushughulisha mwili.

"Ukila wanga na sukari kwa wingi unachosha kongosho lako na kulifanya lifanye kazi zaidi," alisema Dk. Bernard.

Alisema ni muhimu kufanya mazoezi kwa kuwa hurahisisha mzunguko wa damu mwili mzima.

Alieleza kuwa ongezeko la wanaougua ugonjwa wa kisukari kwa watoto na watu wazima kuanzia umri wa miaka 20 hadi 80 na Tanzania watu milioni 1.2 wanaugua na duniani kuna wagonjwa milioni 465.

Bingwa wa Homoni, Joseph Minja, alisema ugonjwa huo unaepukika kwa kubadili mfumo wa maisha na kuzingatia ulaji bora.

# Kituo kipya Mbezi Luis kuanza rasmi Nov. 30

Na Mwandishi Wetu

KITUO kipya cha mabasi yaendayo mikoani na nchi za jirani eneo la Mbezi Luis jijini Dar es Salaam, kitaanza kutumika rasmi mwishoni mwa mwezi huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Sipora Liana, na kuwekwa kwenye mtandao wa halmashauri ya jiji hilo, kituo hicho kitaanza huduma Novemba 30, mwaka huu.

Mkurugenzi huyo amewakumbusha wananchi kuanza kuomba nafasi za kufanya shughuli mbalimbali za kibiashara ndani ya stendi hiyo.

**Pia sehemu za kuhifadhia mizigo, mazoezi, ATM, maeneo ya maduka ya bidhaa za vipuri, vifaa vya michezo, vitambaa, nguo, magodoro, vito, vipodozi, mapambo, saluni, urembo, viatu, nguo za watoto.**

Sehemu ya taarifa hiyo ilieleza kwamba: "Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam anawatangazia wananchi wote kujiandaa kutumia kituo kipya cha mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani kwa huduma za usafiri, usafirishaji, shughuli za biashara, uwekezaji na uchumi katika kituo kipya cha mabasi Mbezi Luis, kuanzia Novemba 30, badala ya kutumia kituo cha mabasi ya Ubungo kinachotumika hivi sasa."

Kuhusu maeneo ya kufanyia biashara, Mkurugenzi huyo aliwataka wananchi kuomba maeneo yakiwamo ya kukatia tiketi, huduma za benki, simu, uwakala na uwakala wa fedha.

Zingine ni maeneo ya maduka ya jumla, supermarket, zahanati, maabara, famasi, migahahawa, vinywaji na baa.

Pia sehemu za kuhifadhia mizigo, mazoezi, ATM, maeneo ya maduka ya bidhaa za vipuri, vifaa vya michezo, vitambaa, nguo, magodoro, vito, vipodozi, mapambo, saluni, urembo, viatu, nguo za watoto.

Taarifa hiyo iliwataka waombaji kutuma maombi yao ya upangishaji kuanzia Novemba 9 hadi 25, mwaka huu, kwa njia ya mtandao kwa kutumia anuani www.pangisha.tamisemi.go.tz

Vilevile, iliwataka baba na mamalishe kuandika barua ya maombi ya kufanya shughuli zao kwenye maeneo yaliyotengwa, kuwasilisha utambulisho kutoka kwa Mtendaji wa Serikali ya Mtaa anapoishi.



Waendesha guta wakiwa wameongozana huku wamesheheni madumu matupu ya plastiki katika Barabara ya Morogoro, eneo la Mwembechai, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Elimu dhidi ya ukatili kijinsia yazaa matunda

Na Yasmine Protace, DODOMA

IMEELEZWA kuwa elimu ya kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia, imezaa matunda.

Imebainishwa kuwa wanaume wanaofanyiwa matukio ya ukatili, wamekuwa wakiyaripoti katika mamlaka husika, ili wahusika wachukuliwe hatua.

Hayo yalisemwa na Amina Mahiya, wakili mtetezi uwajibikaji kutoka Kata ya Kikuyu Kasikazini, Dodoma, alipokuwa akielezea mafanikio ya mradi wa awamu ya pili uliojulikana kwa jina 'Tutimize ahadi', ambapo mradi huo, umetekelezwa na Restless Development.

"Mradi huu wa awamu ya kwanza ilianza mwaka 2018/2019, ambapo awamu ya pili ilianza 2019 mpaka 2020," alisema.

Aliongeza kuwa, mradi ulilenga maeneo ya afya ya uzazi, usawa wa kijinsia, na kwamba ulisimamia maeneo mawili ya ukatili dhidi ya watoto na unyanyasaji wa kijinsia. Alisema katika masuala ya afya ya uzazi, vijana wengi wamekuwa wakidhani masuala ya uzazi ni kwa watoto pekee.

Aliongeza kuwa baada ya kupatiwa elimu, vijana waligundua kuwa afya ya uzazi inahusu makundi yote mawili kati ya wanaume na watoto wa kike.

Alisema hatua hiyo pia ilisaidia vikao kufanyika, ambavyo vitasaidia kuongezeka kwa bajeti katika kituo cha afya, ambapo bajeti hiyo itakuwa ni mkombozi kwa masuala ya uzazi.

Alisema masuala ya kutolewa elimu jamii imeelewa, na kuwa hata wanaume wanafanyiwa ukatili, ambapo wamekuwa wakiyaripo na watuhumiwa wamekuwa wakichukuliwa hatua.

Pia Amina alishukuru ushirikiano walionao na watendaji wa serikali kuanzia ngazi za kata hadi juu, na kuwa wamekuwa msaada mkubwa katika kufanikisha masuala yote ya mradi.

# Wahitimu wa elimu msingi wafundwa

Na Gideon Mwakanosya, SONGEA

WAHITIMU wa elimu ya msingi, wametakiwa kujiepusha na vitendo viovu ambavyo vinaweza kuharibu ndoto zao kielimu na kimaisha wakati huu wanaposubiri matokeo ya mitihani ya darasa la saba iliyofanyika hivi karibuni.

Wito huo ulitolewa na Diwani mteule wa Kata ya Mjini katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma, Mathew Ngalimanayo, wakati wa mahafali ya darasa la saba ya Shule ya Msingi Mashujaa.

Ngalimanayo aliwataka wahitimu hao kuepuka anasa zote za dunia kwa kuwa zinaweza kuwasababishia kushindwa kutimiza malengo yao.

Alisema baada ya kuhitimu masomo, uraiani watakutana na changamoto nyingi za vishawishi, hivyo wanatakiwa kuviepuka na kuvikwepa kwa maslahi ya taifa na wazazi wao waliotumia gharama za kuwasomesha na kuwalea.

"Baada ya mitihani mtakwenda uraiani, kumbukeni huko mwendako kuna mimba za ututoni na Ukimwi upo na unaua, hivyo mnatakiwa kujiepusha na anasa zote za huko uraiani zinazoweza kuchochea tamaa za mwili, dawa za kulevya kwa kuwa taifa linawategemea," alisema Ngalimanayo.

Alisema mafanikio ya shule yoyote ni kuhimiza nidhamu kwa wanafunzi na wanajumuiya wote, hivyo maadili yote mliyoyapata shuleni hapo wayatumie vema popote watakapokuwa.

Pia aliwatahadharisha matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii ambayo yanaharibu maadili ya jamii.

Aidha, akijibu risala iliyosomwa na wahitimu kuhusu changamoto ya uchakavu wa miundombinu ya madarasa, alisema kero hiyo pamoja na changamoto zingine za ufundishaji na ujifunzaji katika shule zote za kata hiyo zitachukuliwa na kufanyiwa kazi.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Vitus Ng'oma, alisema licha ya changamoto mbalimbali wanazokutana nazo lakini mafanikio kitaaluma ni mazuri kwani kwa mwaka 2017 waliofanya mtihani walikuwa 94, waliofaulu walikuwa 91 na waliofeli ni watatu.

Alisema kwa mwaka 2018 waliofanya mtihani walikuwa 101, waliofaulu walikuwa 96 na waliofeli ni watano, na kwa mwaka 2019 waliofanya mtihani ni 88, waliofaulu walikuwa 87 na alifeli mmoja na kwa mwaka huu waliofanya mtihani walikuwa 101.

**Mafanikio ya shule yoyote ni kuhimiza nidhamu kwa wanafunzi na wanajumuiya wote, hivyo maadili yote mliyoyapata shuleni hapo wayatumie vema popote watakapokuwa.**

## Ndivyo kinamama walivyozoa majimbo ya uchaguzi Zanzibar



Ukurasa 12



siasa

JUMATANO NOVEMBA 11, 2020

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

Ukurasa 13

## Abaki mpweke alitoswa na wataalamu, maofisa wengi

# NI MSIBA WA SIASA

## ■Vumbi la uchaguzi lamwachia mbunge kilio
## ■Anaishi gesti, nyumba, magari vyateketezwa

**Sabato Kasika**

LICHA ya vumbi la kimbunga cha uchaguzi mkuu kutulia baada ya kuwapa ushindi wabunge 264 wanaoanza mkutano Dodoma, bado linaendelea kuacha makovu na maumivu kwa wagombea, akiwamo Zuberi Kuchauka, ambaye mali zake zimeharibiwa.

Mbunge wa Liwale (CCM) mkoani Lindi, Kuchauka amebaki na kumbukumbu za uchaguzi zenye machungu kutokana na vitendo vya kuteketezwa nyumba zake mbili na magari matatu.

Katika mazungumzo yake na gazeti hili wiki iliyopita, Kuchauka ambaye kwa sasa anaishi 'gesti' na familia yake, anasema, alishinda kwa kura 50,350, lakini amepata hasara hiyo ambayo hakuitarajia.

Anafafanua kuwa katika nyumba zake hizo, moja alikuwa akiishi na familia yake na nyingine aliweka wapangaji, na kwamba tayari amepata hasara ya Sh. milioni 260.

"Nimeshafungua majalada mawili, katika kituo cha polisi Liwale, kwa ajili ya magari matatu na nyumba mbili zenye Sh. milioni 195 na magari ambayo thamani yake ni. milioni 65 hivyo hasara yote inafikia milioni 260" anasema Kuchauka.

Anasikitika kuwa amehangaika kwa miaka mingi kupata mali hizo, lakini ghafla zimeharibiwa na kubaki na hasara kwa sababu ya watu wasiojua siasa akiomba sheria ichukue mkondo wake.

**ILIVYOKUWA**

Kuchauka anasema, mkasa huo ambao haukudhuru maisha ya mtu ulitokea Oktoba 28, mwaka huu saa 4:00 usiku akiwa katika harakati za uchaguzi.

Waliokuwa wanaishi kwenye nyumba hizo walikimbia lakini hakuna kitu kilichobaki salama, vyote viliteketea.





Nyumba na magari ya Kuchauka ambavyo vimeteketezwa kwa moto. Kuchauka akipiga kura kabla ya mali zake kuteketezwa. **PICHA ZOTE: MPIGA PICHA WETU**

"Wamefanya uharibifu hata kabla ya matokeo ya uchaguzi...walijuaje kuwa wameshindwa? Kama matokeo yangetoka wakiwa wameshinda wangesemaje? Anahoji.

Anasema madai ya waliochoma mali zake ni pamoja na kutoridhishwa na mwenendo wa uchaguzi, kuzuiliwa mawakala wa upinzani kuingia vituoni, kuwapo vituo hewa vilivyo nje ya mfumo na vitambulisho vya kupigia kura.

"Madai ya kubadilishiwa matokeo ya ushindi ya mgombea aliyeshinda na kumpa wa CCM ni maneno ya mkosaji na kama yalikuwa na ukweli, kwanini wasichukua hatua za kisheria? Anahoji.

**UFAFANUZI WA SERIKALI**

Akizungumza na vyombo vya habari hivi karibuni, Mkuu wa Mkoa wa Lindi Godfrey Zambi, anathibitisha kuwapo kwa vitendo hivyo wakati anapotoa taarifa kuhusu uharibifu uliofanywa wakati wa uchaguzi mkuu.

Zambi anasema, katika vurugu hizo, magari zaidi ya saba kati ya hayo mawili ya polisi, majengo ya serikali na ya watu binafsi tisa pamoja na pikipiki moja, vilichomwa moto na kwamba Liwale iliathirika zaidi.

"Wilayani Liwale magari zaidi ya saba, likiwamo la polisi na la binafsi yaliyokodiwa kusaidia uchaguzi yaliharibiwa na kwamba nyumba mbili na magari matatu mali ya Kuchauka yaliharibiwa."

Katika tukio hilo, anasema, imo pia zahanati ya diwani mteule wa Kata ya Liwale Mjini, Omari Mkoyage na nyumba ya polisi wakati wilayani Nachingwea, magari matatu, nyumba, mali za diwani Ahamadi Makoroganya vilichomwa moto.

Anasema wilaya za Kilwa na Lindi katika Halmashauri ya Mtama ziliathiriwa na vurugu hizo, na kwamba polisi inawashikilia watu kadhaa kwa ajili ya mahojiano.

**KUNANI LIWALE?**

Si mara ya kwanza Liwale kukumbwa na vurugu hadi kusababisha uharibifu wa mali za mamilioni ambazo zinahusishwa na uhasama wa kisiasa.

Ilikuwa ni mwanzoni mwa mwaka 2013, ghasia zilizuka katika Kijiji cha Liwale B na kusababisha kuteketezwa kwa mali nyingi, wizi, uharibifu na kuuawa kwa mifugo, zilitokana na wakulima kudai kupunjwa malipo ya korosho.

Inadaiwa, wakulima wa korosho walianzisha vurugu hizo wakitaka kulipwa nusu ya mwisho ya fedha za mauzo katika Chama cha Ushirika Mnali kwa Sh1, 200 lakini chama kikapanga kuwalipa Shilingi 200.

Aliyekuwa mbunge wa Liwale wakati huo, Faith Mitambo (CCM), naye aliathiriwa na vurugu hizo, kutokana na nyumba zake kuteketezwa kwa moto.

"Haya ya korosho ni kama njia tu, hapa zimetumika siasa kuna mkono wa siasa hapa, kama si siasa ni nini? Kwa nini walioathiriwa ni wanachama wa CCM tu? Anahoji Mitambo wakati huo. Katika tukio hilo, mbunge huyo alichomewa nyumba mbili na moja ikiteketea na wengine waliochomewa nyumba ni Mwenyekiti wa Chama cha Msingi cha Ushirika cha Umoja, Hassan Myao.

Aidha, Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Hassan Mpako, diwani wa viti maalumu CCM Liwale, Amina Mnocha, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, Abbas Chigogola, Mwenyekiti wa CCM Liwale, Mohamed Ng'omambo na Katibu Mwenezi wa CCM Liwale, Abdallah Chande, wote walikumbukwa na kadhia hiyo.

Katika tukio hilo, nyumba zaidi ya 20 nyingi zikiwa za viongozi wa CCM na vyama vya msingi, ziliteketezwa kwa moto, huku polisi mkoani Lindi ikinasa watu 50 kwa tuhuma za kuhusika na tukio hilo.

# Ndivyo kinamama walivyozoa majimbo ya uchaguzi Zanzibar

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

"MSHINDI ni Mwanaasha Khamis,... mbunge mteule ni Mtumwa Peya... mwaka huu mbunge wa jimbo la Mfenesini ni Zubeda Khamis..." Ndizo sauti za wasimamizi wa uchaguzi zilivyohanikiza ndani ya majimbo 12 ya Zanzibar wakati wa kutangaza matokeo ya uchaguzi mkuu uliofanyika mwisho wa mwezi uliopita na kushuhudia wanawake zaidi wakiibuka kidedea.

Mwaka huu idadi ya wanawake waliotangazwa kushinda uchaguzi mkuu majimboni ni 12 ikilinganishwa na saba walioibuka kidedea mwaka 2015 kwa nafasi za uwakilishi na ubunge, mafanikio yanayotajwa kuwa ni kutokana na juhudi mbalimbali za wanaharakati katika kuihamasisha jamii kuwaunga mkono wanawake wanaogombea nafasi za uongozi majimboni.

Pia juhudi kubwa zimefanywa na baadhi ya vyama vya siasa ambazo ilani zake zimeweka bayana wanawake kushiriki katika nafasi za kugombea uongozi ili kuingia katika vyombo vya kutunga sheria likiwamo Bunge la Jamuhuri ya Muungano na Baraza la Wawakilishi.

Miongoni mwa kinamama walitetea nafasi ya uwakilishi jimbo la Bubwini ni Mtumwa Peya, anayesema siri ya ushindi wake ni kushirikiana na wananchi wa jimbo hilo bila kujali itikadi za kisiasa na kufanyakazi za maendeleo.

Anasema tangu kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi na uchaguzi mkuu wa vyama vingi wa kwanza mwaka 1995 jimbo la Bubwini limeongozwa na wanaume pekee na mabadiliko yamekuja mwaka 2015 kutokana na jamii kubadili mitizamo na kuamini kuwa mwanamke anaweza kuongoza ikipewa fursa.

"Naipongeza CCM chama changu pamoja na wananchi wa Bumbwini kwa kuniamini na kunipa ridhaa tena kwa kipindi cha miaka mitano mingine baada ya kushika usukani kwa miaka mitano iliyopita",anasema Paye.

Mwakilishi huyo mteule anatoa ahadi za kutekeleza ilani ya CCM na kuleta maendeleo kwa wananchi wa jimbo hilo huku akiwataka wanawake kujipanga na kujiunga na vikundi vya ushirika na uzalishaji mali ili wanufaike na mikopo na mipango ya maendeleo.

Mwanaasha Khamis Juma ni mwakilishi mteule wa jimbo la Dimani, anasema hana jingine ila kuwatumikia wananchi wa jimbo hilo na kuzitatua changamoto mbalimbali zinazowakabili.

Anaahidi upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama ili kuwapunguzia wanawake mzigo wa kutembea masafa marefu ya kusaka maji : "Tatizo la uhaba wa maji linawasumbua zaidi kinamama kwa sababu wao ndiyo wanaofanya shughuli mbalimbali katika familia zao ikiwamo kufua nguo, kufanya usafi, kupika na mambo mengine ambapo bila ya maji mambo hayo hayawezi kufanyika."



Mwakilishi mteule jimbo la Bumbwini, Mtumwa Peya (kulia) akitambulishwa kwa wananchi wakati wa mkutano wa kampeni na meneja wa kampeni Mariyam Muharami Shomari. **PICHA MWANDISHI WETU.**

Mwanaasha anakuwa ni mwakilishi wa kwanza mwanamama katika jimbo la Dimani ambapo tangu uchaguzi wa mwaka 1995 jimbo hilo linaongozwa na wanaume pekee kwa nafasi ya uwakilishi na ubunge.

Mwanaasha anakubalika na wapigakura tofauti ambapo awali alikuwa mwakilishi wa jimbo la Chukwani lakini Tume ya Uchaguzi ilipofanya marekebisho na kulifuta jimbo hilo alilazimika kujitosa katika jimbo la Dimani kugombea nafasi hiyo.

Mwanaasha anawashinda vigogo kadhaa wakiwamo mawaziri waandamizi serikalini lakini haikuwa kikwazo cha kuukwaa ushindi.

Kisiwani Pemba, wanawake hawako nyuma, wagombea watano wameweka rekodi ya kunyakua nafasi za uwakilishi na ubunge majimboni, kwa jimbo la Pandani Mariyam Issa, aliibuka na ushindi akiwa mbunge kupitia Chama cha Wananchi CUF.

Mariyam anakuwa wa kwanza kupitia chama hicho kupata nafasi hiyo ambayo ilikuwa ikigombewa na wanasiasa mbalimbali, ikumbukwe kuwa tangu uchaguzi wa mwaka 1995 chama cha CUF kilipopata mbunge mwanamama jimbo la Chakechake Fatuma Maghimbi, haikuwahi kupata nafasi nyingine yoyote kwa wanawake wakati wote uwakilishi na ubunge ulishikiliwa na wanaume kipindi chote Pemba ikiwa ni ngome kuu ya wapinzani.

Mwakishi mwingine ni Harous Said Suleiman, ambaye sasa ataungana na wanawake wenzake kutetea masuala mbalimbali ya kinamama katika vyombo vya kutunga sheria.

> "Suala la wanawake kushika nafasi za uongozi katika CCM halina pingamizi tumeona uwezo wao ndiyo maana chama kimewateuwa kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi mkuu,"anasema Nao.

Harous ndiye mwakilishi mteule wa jimbo la Wete kupitia CCM anayetetea nafasi yake hiyo kwa kipindi cha pili ambapo uongozi uliopita wa Dk Ali Mohamed Shein, alikuwa pia ni Naibu Waziri wa Afya Zanzibar.

Mwanamke mwengine ni Zubeda Khamis Ubunge mteule wa jimbo la Mfenesini kwa mara ya kwanza amegombea jimbo hilo na kushinda.

Zubeda anawaangusha vigogo na wanasiasa wakongwe waliogombea nafasi ya ubunge jimbo hilo akiwamo mbunge aliyemaliza muda wake.

Zubeda anakipongeza chama chake pamoja na wananchi wa jimbo la Mfenesini kwa kumchagua na kumuamini hivyo aliwaahidi kuwaletea maendeleo.

"Nitahakikisha nawaletea maendeleo wana Mfenesini hivyo kama mlivyonipa ushirikiano kipindi chote cha kampeni nawaombeni mwendelee kunipa ushirikiano ili niwaletee maendeleo'anasema.

Wanawake wengine waliong'ara katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu ni Wawakilishi wa CCM kutoka Pemba ni pamoja na Mariyam Thani Omar, mwakilishi jimbo la Gando , Zawadi Amour Nassor mwakilishi mteule jimbo la Konde , Bahati Khamis Kombo jimbo la Chambani ,Asha Abdallah Mussa uwakilishi jimbo Mahonda, Rukia Omar Mapuri mwakilishi jimbo la Amani.

Wengine ni Mwantakaje Juma mbunge jimbo la Bububu na Mwanakhamis Kassim Said jimbo la Magomeni.

Katibu wa Idara ya Itikadi na Uenezi wa Kamati Maalum ya CCM Zanzibar, Catherin Peter Nao, anasema ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020/2025 imetoa kipaumbele kwa wanawake kushika nafasi za uongozi na kufikia asilimia 50/50 kuingia katika vyombo vya kutunga sheria.

"Suala la wanawake kushika nafasi za uongozi katika CCM halina pingamizi tumeona uwezo wao ndiyo maana chama kimewateuwa kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi mkuu,"anasema Nao.

Kiongozi wa timu ya wanaume wa mabadiliko Mohammed Jabir, anasema wakati umefika sasa kwa jamii kuwa na mtizamo mwenye sura ya mabadiliko kwa mwanamke kwamba anauwezo mkubwa wa kuongoza.

Alisema zipo tafiti mbalimbali zilizofanywa wanawake walioshika nafasi za uongozi wamefanya vizuri na kukubalika na makundi mbalimbali ya kijamii na kuongeza:

"Wanawake wana uwezo wa kuleta mabadiliko ya kijamii katika sekta mbalimbali kama watapewa nafasi za kushika katika uongozi."

Kwa upande wake Shekhe Khamis Abdulkhamid, anasema Uislamu umewapa hadhi wanawake katika kuongoza na hata maandiko matakatifu yanamuelezea mwanamke kuwa ni kiongozi.


"Hakuna pingamizi kwa mwanamke kuwa kiongozi katika dini hata zipo baadhi ya aya katika kitabu chetu kitakatifu ikiwamo Suratul Mujadila ambayo inaelezea uwezo wa mwanamke katika kutetea haki na kumtukuza,"anasema Abdulkhamid.

TRUMP CHALI

# Abaki mpweke alitoswa na wataalamu, maofisa wengi

•Lakini Republican wababe, waendelea kuwa wengi kwenye Senate

•Wimbi la mageuzi kunusuru weusi 'black lives matter' mashakani



Rais Trump muda mfupi baada ya kukubali kushindwa kwenye uchaguzi wa Novemba 3, 2020. **PICHA MTANDAO.**

**Na Ani Jozeni**

MAELFU ya raia wa Marekani walijazana katika barabara za miji mikubwa na vitongoji Jumamosi iliyopita usiku kusherehekea kung'olewa madarakani kwa Rais Donald Trump, wa chama cha Republican baada ya mashirika makubwa manne ya habari ikiwamo tevisheni ya CNN na Associated Press (AP) kuafikiana kuwa kura zilizobaki kuhesabiwa katika baadhi ya majimbo hazitatosha kumrudisha Trump ikulu ya Washington DC.

Hadi wakati huo kura zilizokuwa zinangojewa ni za jimbo la Pennsylvania ambazo zilielezwa kuwa hazitoshi kubadili mwenendo wa Joseph Biden wa chama cha Democrats kushinda viti 20 vya jimbo hilo ili kufikisha kura 270 za majimbo maarufu kama 'electroral colleges '. Idadi hiyo ikifikiwa hata kama yapo majimbo hayajamaliza kuhesabu kura mshindi anatangazwa bila kigugumizi.

Wachambuzi wa siasa waliokuwa wakijadiliana hisia za raia wa Marekani walisema kuwa jambo la msingi halikuwa matazamio ya mabadiliko kisera, ila zaidi kumuondoa Trump. Ni kiongozi mpambanaji aliyewaudhi wengi, asiyeaminika kwa kile anachosema na mara nyingi anakinzana na uhalisia wa vitu na zaidi kuonekana kupuuza ugonjwa wa corona, kutoshabikia uvaaji wa barakoa na kuonekana kuwa anaunga mkono polisi wabaguzi wanaowatwanga risasi na kuwaua watuhumiwa weusi ovyo.

Walichoshangaa wachambuzi wa kisiasa wa nchi hiyo ni matokeo licha ya kuwa takriban kila kundi Marekani lilikuwa na ugomvi huu au ule na Trump na katika wiki za mwisho wachumi mashuhuri 700, wakiwamo saba wa tuzo ya Nobel waliwataka Waamerika kumpigia kura Joe Biden. Isitoshe, miaka minne baada ya maofisa 50 waliokuwa na wadhifa wa ushauri kuhusu usalama wa taifa katika ikulu ya Marekani kusema kuwa Trump asingefaa kuongoza nchi hiyo, walitoa waraka mwingine kusema kuwa urais wake umekuwa mbaya kuliko walivyohofia. Na bado Biden amemshinda Trump kwa kura milioni 4.1 au asilimia 2.7 hali inayoonyesha wafuasi wa Trump hawakusikiliza wakosoaji.

Kutokana na chuki inayoshangaza kwa Trump kwa vile anaonyesha kutokujali yale ambayo 'liberals,' watu wenye siasa 'poa' kuhusu masuala ambayo wahafidhina wanaona ni ya msingi sana, ilitazamiwa kuwa Democrats (kupitia kwa mgombea wao Biden) wangekamata pia senate pamoja na ikulu.

> Shangwe ya kuongezea Baraza la Wawakilishi ambalo lilikuwa na wingi wa Democratic katika muhula huo mmoja wa Trump, hawakufanikiwa na idadi yao ya wabunge (wawakilishi) itapungua ukilinganisha na awali, na isitoshe, wachambuzi wanasema waliochaguliwa kutoka Republican safari hii ni wakali kuliko wa awali.

Shangwe ya kuongezea Baraza la Wawakilishi ambalo lilikuwa na wingi wa Democratic katika muhula huo mmoja wa Trump, hawakufanikiwa na idadi yao ya wabunge (wawakilishi) itapungua ukilinganisha na awali, na isitoshe, wachambuzi wanasema waliochaguliwa kutoka Republican safari hii ni wakali kuliko wa awali.

Ina maana kuwa licha ya shangwe za mamilioni ya raia wa Marekani kufurahia kuondoka madarakani Rais Trump, hapatakuwa na shangwe katika kazi ngumu ya kutawala, kwani kwa kiwango cha ufaulu wa Trump kuweka muhuri katika taasisi muhimu za mfumo wa siasa wa Marekani itakuwa kazi ngumu sana kubatilisha. Hatua ya kwanza ni hiyo ya senate, kuwa ni mabadiliko tu yanayokubaliwa na maseneta wa Republican yatakayopitishwa, na siyo yale yasiyokubalika kwao, ambayo ina maana kuwa mipango yote ya 'Black Lives Matter' kuhusu urekebishaji wa uendeshaji polisi utabaki serikali za majimbo. Halafu, mipango ya nishati mbadala itabidi iendane na matakwa ya kutoongeza kodi hata kama kutakuwa na mabadiliko ni kidogo.

Eneo jingine ambako alama ya Trump itadumu na siyo kwa mipango yake mwenyewe ila ni wazi kuwa 'nyota' zilikuwa upande wake, ni kuweza kuteua majaji watatu Mahakama ya Juu ambao wakishateuliwa wanatumikia maisha yao yote. Katika miezi miwili ya mwisho wa muhula wake, alifariki Jaji Ruth Bader Ginsburg, Democratic wakapiga kelele eti Trump asitaje wa kujaza nafasi hiyo, huku wakijua wangefanya hivyo wangekuwa madarakani. Alimtaja akapitishwa, sasa wahafidhina wana wingi wa 6-3 Mahakama ya Juu, tayari kuvunja miiko ya uliberali kuhusu utoaji mimba, au ushoga.

Kwa vile alishaonyesha tangu mwanzo kuwa itakuwa vigumu kwake kukubali matokeo kama bado kuna utata wowote kuhusu kuhesabu kura, ilitazamiwa kuwa Trump akishindwa kutakuwa na patashika. Eneo la kwanza tayari ameshashindwa, kwani ilipothibitika kuwa kura zilizobaki kuhesabiwa Pennsylvania hata angezipata zote haziwezi kumpa ushindi jimbo hilo, kurudia kuhesabu kura Georgia kama watawala wa ki-Republican wa jimbo hilo walivyokuwa wanataka, kulikuwa tayari kumepoteza ladha. Majimbo kadhaa yalitupilia mbali madai ya mawakili wa Trump kuwa kura zilizokuwa zinaendelea kuhesabiwa hazikuwa halali, ambayo ni Georgia, Florida, Pennsylvania na Michigan.

Ambacho pia kimedhihirishwa katika uchaguzi uliomalizika ni kuwa nguvu ya Trump miongoni mwa wapiga kura Wazungu na hasa katika maeneo yenye mashamba makubwa na uwakilishi mkubwa bungeni (ukilinganisha na idadi ya watu) ni kubwa sana. Licha ya kuwa viongozi wengi wa Republican bungeni hawakuwa wanaunga mkono madai yake ya kuvurugwa kura, bado hakuna aliyehoji neno lolote, hata kiongozi wa Republican katika senate, Mitch McConnell, akasema 'kura zote halali zihesabiwe,' wakati hapakuwa na ushahidi wowote wa kura batili. Ina maana kuna moto ataanza kuuwasha Trump hadi akabidhi madaraka Januari 20, na siyo ajabu wafuasi wake hasa miongoni mwa polisi wakaanza visasi.

Kuhusu hatma ya Iran, China na mashirika kadhaa ya Umoja wa Mataifa ambako utawala wa Trump ulijitoa au unakwamisha shughuli zake, haitakuwa rahisi kwa mteule Biden kurudisha ule mkataba wa kuzuia Iran kuwa na silaha za nuklia na hivyo iondolewe vikwazo, wakati inaendesha vita kote Mashariki ya Kati, dhidi ya Marekani, Israel na marafiki zao. Wala haitakuwa rahisi kuondoa vizuizi ilivyowekewa China halafu viwanda vipukutike zaidi kuelekea China.

Shirika la Biashara Duniani (WTO) litaendelea kuhangaika kwani Biden anaweza asitake kuiudhi Senate kwa kuondoa zuio (veto) kuhusu kuchaguliwa kwa Dk. Ngozi Okonjo-Iweala, Waziri wa Fedha wa zamani Nigeria, kuwa mkurugenzi wake mkuu. Pia anaweza kuirudisha Marekani uanachama katika Shirika la Afya Duniani (WHO) ila siyo mkataba wa mazingira kuhusu tabia nchi. Akijaribu kurudisha mkataba huo inawezekana akakwama kwenye senate.

# Hawa ndiyo viongozi vibabu Afrika 2020

## •Kikongwe zaidi ni Beji Caid Essebsi wa Tunisia

**Na Mwandishi Wetu**

KABLA ya Robert Mugabe, kuondolewa ikulu na Makamu wake Emerson Munangagwa, alikuwa na sifa moja kuu kwamba ndiye aliyekuwa Rais kikongwe barani Afrika.

Baada ya Mugabe au Jongwe kufutwa kazi ya utumishi wa umma ikulu ya Harare, kiti cha rais mzee kuliko wote Afrika na wa pili kwa umri mkubwa duniani ambaye bado yuko madarakani, kinakaliwa na Rais Beji Caid Essebsi wa Tunisia.

Essebi aliyezaliwa miaka 92 iliyopita itakapofika Novemba 29 mwaka huu ataadhimisha miaka 93 ya kuzaliwa kwake kwani alikuja duniani mwaka 1926.

Ndiye rais wa kwanza wa kuchaguliwa nchini Tunisia kwa mchakato wa uhuru na haki . Aliibuka kidedea mwaka 2014 akiwa na miaka 87.

Kabla ya uteuzi alikuwa Waziri wa Mambo ya nje kuanzia mwaka 1981 hadi 1986 kisha Waziri Mkuu kuanzia Februari 2011 hadi Desemba 2011.

Rais mzee kuliko wote duniani lakini anayeendelea kuongoza ni Karolos Papoulias aliyezaliwa Juni 4, 1929 na anaendelea kuiongoza Ugiriki na chama chake ni Panhellenic Socialist Movement.

**BIYA CAMEROON**

Nani zaidi kwa uzee? Ni babu Paul Biya, Rais wa Cameroon na miongoni mwa marais mzee zaidi barani hapa akiwa amefikisha miaka 85 ndiyo kwanza kumekucha hajafikiria kung'atuka.

Paul Biya aliyezaliwa Februari 13, 1933 ni mwanasiasa damu na amekuwa Rais wa Cameroon kuanzia Novemba 1982, akiwa na miaka 85 bado ni yuko ikulu akiwa ni wa pili kwa ukongwe Afrika na wa saba kwa kuwa na umri mkubwa duniani kwenye orodha ya marais 10 bora wazee duniani.

**BOUTEFLIKA NA ALGERIA**

Abdelaziz Bouteflika ni babu anayeiongoza Algeria, ametimiza miaka 81 akizaliwa Machi 2, 1937.

Abdelaziz Bouteflika mkongwe wa Algeria ni rais wa tano wa nchi hiyo akishika usukani kuanzia 1999.

Ametumikia nafasi mbalimbali kama Waziri wa Mambo ya Nje kuanzia 1963 hadi 1979.


Aidha, amekuwa Rais akichukua uongozi baada ya vita vya wenyewe kwa wenyewe mwaka 2002 na kumaliza utawala wa dharura Februari 2011 japo taifa hilo lilikuwa na hali tete kiusalama.




Rais Beji Caid Essebsi wa Tunisia



Paul Biya wa Cameroon



Alpha Conde wa Guinea



Manuel Pinto da Costa ni Rais wa Visiwa vya São Tomé and Príncipe

Bouteflika ambaye pia amewahi kuwa Rais wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, anakuwa mmoja wa marais wazee Afrika na duniani.

**VISIWA VYA SAO TOME**

Babu mwingine ni Manuel Pinto da Costa ni Rais wa Visiwa vya São Tomé and Príncipe akiwa na miaka 81, alizaliwa Agusti 5, 1937.

Manuel Pinto da Costa kitaaluma ni mchumi mbobezi na mwanasiasa ambaye kwa mara ya kwanza alikuwa rais wa São Tomé and Príncipe kuanzia mwaka 1975 hadi 1991.

Kwa mara nyingine alichaguliwa kuwa rais mnamo Agosti 2011 na kuendelea kuiongoza nchi hiyo kuanzia Septemba 3, 2011.

**CONDE WA GUINEA**

Mwingine ambaye ni mzee ni Rais Alpha Conde wa Guinea. Hivi karibuni Mahakama ya Katiba ya Guinea ilimthibitisha kuingia ikulu kwa awamu ya tatu.

Aidha, mahakama inakubaliana na ushindi wake wa kishindo kwenye uchaguzi uliopingwa na kukataliwa na wapinzani wake kwa madai ya kugubikwa na rushwa na udanganyifu mkubwa.

Conde mwenye miaka 82 anashika namba tano kuwa rais kikongwe wa Afrika ambaye ameanza kuiongoza Guinea kuanzia mwaka 2010, alibadili katiba ili aendelee kuwa rais licha ya kwamba katiba inamtaka kukaa awamu mbili ikulu.

**Africa Business Agency**



# Umuhimu uwekezaji elimu watoto wa kike wahimizwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JAMII imetakiwa kuwekeza kwenye elimu ya watoto wa kike, ili kuwasaidia kutimiza ndoto zao, badala ya kuwaozesha katika umri mdogo kwa tamaa za kupata mali.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi isiyokuwa ya Kiserikali ya Action Girls Foundation (AGF), Rabia Mussa, alitoa rai hiyo jana alipokuwa akizungumza kuhusu watoto wa kike kukatizwa ndoto zao.

Alisema kuna umuhimu wa jamii kubadilika ili kuyakabili matatizo mbalimbali yanayosababisha watoto wa kike kukatisha masomo yao kutokana na kupata ujauzito.

Mussa alisema kuwa wazazi lazima wafikirie kuwekeza kwenye elimu ya watoto wao na kuwaozesha wakiwa na umri mdogo na kufifisha ndoto zao.

**Vitendo vya ukatili hufanyika kwa watoto, lakini changomoto iliyopo ni kutishiwa maisha na wanaowafanyia vitendo hivyo jambo ambalo husababisha taarifa nyingine za ukatili kutojulikana.**

Alifafanua kuwa, kumekuwa na matatizo mengi ambayo yanawakabili watoto wa kike lakini mengi yanatatulika kama kutakuwa na ushirikiano wa kutosha.

Alisema pia wanaandaa programu za kuzuia na kudhibiti visababishi vinavyosababisha wasichana kupata mimba, kwa kusaidia kujenga uelewa wa wazazi na jamii juu ya umuhimu wa kuzungumza na watoto wa wao, ikiwamo kuwapa uhuru wa kujieleza matatizo yao.

Alisema tatizo jingine linazowakabili watoto wa kike ni uwepo wa mahusiano ya kimapenzi kati ya wanafunzi na walimu, ushirikiano mdogo kati ya wazazi na walimu, upungufu mkubwa wa matundu ya vyoo na madawati.

Naye mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Mounti Igovu, wilayani Mpwapwa, Nairati Mlewa, alisema baadhi ya watoto wa kike wamekuwa wakinyimwa haki zao za msingi ikiwamo kupata elimu na wengine kupoteza maisha kwa ajili ya vitendo vya ukatili ikwamo kubakwa.

"Vitendo vya ukatili hufanyika kwa watoto, lakini changomoto iliyopo ni kutishiwa maisha na wanaowafanyia vitendo hivyo jambo ambalo husababisha taarifa nyingine za ukatili kutojulikana," alisema.

Alisema kama jamii ikitoa kipaumbele kwenye malezi na elimu kwa watoto wa kike, kutapunguza changamoto nyingi zinazowakabili.

Alisema kuwapo kwa mashirika ya kiserikali yanayofanya kazi ya kutetea haki za watoto wa kike kwa kiasi kikubwa kumesaidia wengi wao kutambua haki zao za msingi ikiwamo kupata elimu.

# Machinga wapewa mbinu ya biashara

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAFANYABIASHARA ndogo, wametakiwa kufanya biashara zao kwa malengo ya kukuza mitaji na kuacha kupandisha bei za bidhaa bila mpangilio katika masoko panapokuwapo na mahitaji makubwa sokoni.

Ofisa masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, alitoa ushauri huo jana wakati akizungumza na wafanyabiashara hao, alipofanya ziara ya kuwatembelea na kuona bidhaa wanazouza katika masoko mbalimbali ya Jiji la Dodoma.

Alisema badala ya kuendelea kupandisha bei bidhaa zao, ni vema wakaangalia upande wa pili wa kufanya biashara hizo kwa malengo ya kukuza mitaji ikiwa ni pamoja na kujiletea kipato.

Yuna alisema Jiji la Dodoma limekuwa makao makuu ya serikali, hivyo kuna fursa nyingi zinajitokeza ambazo zinawapatia kipato kutokana na biashara wanazozifanya.

Aliwataka, wafanyabiashara hao kutumia fursa hiyo kukuza mitaji yao, badala ya kutumia mwanya huo kwa kupandisha bei za bidhaa bila mpangilio.

"Hivi sasa baadhi ya matatizo mbalimbali yaliyokuwa yakiwakabili, miongoni mwa wafanyabiashara ndogondogo tayari kwa upande wa serikali kupitia halmashauri ya jiji, imeanza kutatuliwa hii ni pamoja na kutengewa maeneo yaliyo salama kwenu nyinyi na hata kwa wateja wenu," alisema.

Awali, wafanyabiashara hao, wakizungumza mbele ya ofisa masoko huyo, walisema pamoja na malengo waliyonayo ya kutaka kujiinua kiuchumi na kukuza mitaji yao wana kero zinazowafanya kutopiga hatua.

Juma Abdalah, anayefanya shughuli zake soko la Chang'ombe Jiji la Dodoma, alitaja kero hizo ni pamoja na maeneo mengi kutokuwa rafiki kwao.

Halima Hassani, mamalishe wa soko la Kikuyu Jiji la Dodoma, aliwataka wajasiriamali wanaojishughulisha na upikaji wa vyakula, kuzingatia masharti ya afya ili kuwalinda wateja wanao wahudumia pamoja na wao.

Alisema kuwa wengi wao bado mazingira yao siyo rafiki kwa walaji na kwao, hali ambayo inaweza kusababisha kuwapo kwa mlipuko wa magonjwa hasa katika kipindi hiki cha mvua za vuli.



Waziri Mkuu mstaafu na Mbunge wa Jimbo la Ruangwa, Kassim Majaliwa, akiapa kuwa mbunge wa jimbo hilo, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

# TAG yataka walioshindwa uchaguzi mkuu kuombewa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KANISA la Tanzania Assemblies of God (TAG) limewaomba viongozi wa dini na Watanzania kwa ujumla kuwaombea watu wote walioshindwa katika uchaguzi mkuu wa 2020.

Askofu Mkuu wa Kanisa la TAG, Dk. Barnabas Mtokambali, aliyasema hayo jijini hapa alipokuwa akizungumza kwenye mahafali ya 38 ya Chuo cha Biblia Kanda ya Kati (CBC).

Askofu huyo alisema baada ya matokeo kutangazwa na wao kutofanikiwa kushinda, ni dhahiri kuwa wapo kwenye kipindi kigumu, lakini wanapaswa kukubaliana na hali halisi na kuendelea na shughuli nyingine.

"Uchaguzi umepita toka Oktoba 28, mwaka huu kwa ajili ya kuwachagua madiwani wabunge na Rais, nafasi zote wameshapatikana ikiwamo Rais kuapishwa ili kuwatumikia wananchi kwa kipindi kingine cha miaka mitano," alisema Askofu.

Dk. Mtokambali ambaye ni Rais wa makanisa ya TAG Barani Afrika, alisema kila mtu ana wajibu wa kuwaombea ili Mungu aondoe maumivu na uchungu waliyonayo ambayo yalisababishwa na uwekezaji wa nguvu na mwili waliyokuwa wameufanya katika uchaguzi mkuu.

Alisema kibinadamu watu hao wapo kwenye kipindi kigumu ambacho kinasababisha kukata tamaa, kuwapo kwa mkanganyiko wa mambo yao yanaweza kuathiri haki zake za msingi.

"Tuna wajibu wa kuwaombea ili wasikate tamaa ya kugombea awamu nyingine zijazo," alisema Dk. Mtokambali.

Hata hivyo, aliwataka viongozi hao wa dini waliohitimu kumpa Mungu nafasi ya kwanza katika utendaji kazi wao, kuweka bidii katika kutimiza uhodari wa kuwatumikia Watanzania.

Alisema wanatakiwa kuwa na maono makubwa kufikisha huduma hadi vijijini, kutembea katika sheria na kanuni za kanisa ikiwamo kuwatii viongozi wao.

Mkuu wa chuo hicho, Jonas Mkoba, alisema hawatarajii kusikia malalamiko yanayohusu wahitimu hao kuhusu utendaji kazi wao, badala yake wafanye kazi wakiwa na ari waliyotoka nayo chuoni.

Mkoba, alisema wahitimu hao 110, wamesomeshwa kwa ufadhili wa kanisa hilo, huku akiwaomba wadau wengine kijitokeza ili kusaidia uenezaji wa neno la Mungu kupitia watumishi wanaosomeshwa katika chuo hicho.

Wahitimu hao 110 wa elimu ya biblia ni wa ngazi ya astashahada, stashahada, shahada na shahada ya uzamili.





# Uzalishaji tumbaku Chunya kupanda

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

UZALISHAJI wa tumbaku katika Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, unatarajiwa kuongezeka kutoka kilo milioni za msimu wa 2019/20 mpaka kufikia kilo milioni 10.6 katika msimu ujao wa kilimo.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Simon Mayeka, alisema jana ofisini kwake kuwa makadirio ya kuongezeka kwa uzalishaji huo yanatokana na mahitaji makubwa ya wanunuzi wa zao hilo kuu la biashara wilayani hapa.

Alisema kwa utamaduni wa kilimo cha tumbaku, kila mwaka wanunuzi hubainisha mahitaji yao kabla ya msimu wa kilimo kuanza ili wananchi wanapolima wanakuwa na uhakika wa soko na kuzalisha kulingana na kiwango kinachohitajika.

**Bei ya tumbaku mwaka huu pia itaongezeka kidogo. Kwa sasa ni mapema kusema, lakini wakati utakapofika tutawatangazia wakulima.**

"Mwaka huu makadirio yanaonyesha kuwa kutakuwapo na ongezeko la mahitaji ya tumbaku kwa wadau wetu. Hii ni fursa kwa wakulima wetu kupanua mashamba yao ili kuongeza uzalishaji utakaokidhi mahitaji ya wanunuzi wa zao hilo," alisema Mayeka.

Aidha, alisema bei ya zao hilo pia inatarajiwa kupanda kidogo ikilinganishwa na bei waliyouza msimu uliopita ambayo ilikuwa ndogo kutokana na matatizo yaliyosababishwa na mlipuko wa virusi vya corona.

"Bei ya tumbaku mwaka huu pia itaongezeka kidogo. Kwa sasa ni mapema kusema, lakini wakati utakapofika tutawatangazia wakulima," alisema Mayeka.

Baadhi ya wananchi hususan wakulima wa tumbaku wilayani Chunya, wamepokea taarifa hiyo kwa shangwe na kuishukuru serikali pamoja na viongozi wapya waliochaguliwa hivi karibuni kwa kuonyesha dalili njema ya kuwaletea mafanikio kwenye kilimo cha zao hilo.

Mmoja wa wakulima hao, Daudi Mpigauzi, alisema ongezeko hilo linatoa wigo mpana kwa wakulima kupanua kilimo cha tumbaku akidai kuwa ndilo zao pekee la biashara wanalolitegemea.

"Kitendo cha kuturuhusu kuongeza uzalishaji wa tumbaku kwetu ni neema kubwa kwa sababu tunapata fursa ya kupanua mashamba ili kuongeza uzalishaji huku tukiwa na uhakika wa soko la mazao yetu," alisema Mpigauzi.

Hata hivyo Mpigauzi aliomba serikali inapohamasisha kuongeza uzalishaji wa zao la tumbaku ikumbuke na kuongeza bei ili kumnufaisha mkulima wa zao hilo.

Wilaya ya Chunya yenye tarafa mbili za Kiwanja na Kipembawe, kiuchumi inategemea tumbaku na uchimbaji wa madini. Tumbaku inazalishwa zaidi tarafa ya Kipembawe, huku dhahabu ikichimbwa zaidi katika Tarafa ya Kiwanja.




Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, akipanda mkorosho nje ya Kituo cha Polisi cha wilayani Mbarali, kilichojengwa na kampuni ya Mbarali Estate, eneo la Ubungo, Kata ya Ubaruku, wilayani Mbarali hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Serikali yawataka wakulima chikichi kukaa mkao wa kula

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

WIZARA ya Kilimo imeiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya kuwaandaa wakulima kupokea mbegu za kisasa za chikichi kwa ajili ya kupanda kwenye mashamba yao.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao kutoka Wizara ya Kilimo, Nyasebwa Chimagu, akiwa katika ziara ya kikazi wilayani hapa.

Nyasebwa alisema agizo hilo ni utekelezaji wa mkakati wa serikali wa kuongeza uzalishaji wa zao hilo ambalo linatarajiwa kuliwezesha taifa kujitosheleza kwa mafuta ya kula.

Alisema kwa sasa serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Naliendele, Mtwara, imeanza uzalishaji wa mbegu bora za chikichi mkoani Kigoma ambazo zinatarajiwa kusambazwa katika maeneo yote yanayozalisha zao hilo.

"Kyela ni miongoni mwa maeneo ambayo mbegu bora zinazozalishwa na serikali huko Kigoma zitaletwa kwa ajili ya kupanua uzalishaji wa chikichi. Sasa ni wajibu wenu kama halmashauri kuwaandaa wakulima kuzichukua mbegu hizo zitakapokuwa zimefika ili wakapande kwenye mashamba yao," alisema Chimagu.

Alisema ingawa mbegu nyingi za chikichi zinazalishwa mkoani Kigoma, serikali kupitia Wakala wa Mbegu (ASA) kwenye kituo chake cha Mbozi pia imeandaa uzalishaji wa mbegu bora za chikichi ambazo zitasambazwa katika ukanda wa Nyanda za Juu Kusini.

Ofisa Kilimo wa Kata ya Itope, Stellah Mwakaje, alisema Halmashauri ya Wilaya ya Kyela kwa kushirikiana na TARI wameandaa shamba la mbegu bora za chikichi katika kijiji cha Kikusya wilayani Kyela ambalo pia linatarajiwa kurahisisha upatikanaji wa mbegu bora kwa wakulima.

Akizungumzia utekelezaji wa mkakati huo, Ofisa Kilimo Wilaya ya Kyela, Kenneth Nzilano, alisema tayari wameandaa shamba lingine lenye ukubwa wa ekari 13 lililoko Kata ya Makwale wilayani hapa ambalo litatumika kama shamba darasa ili kuwafundisha wakulima kilimo cha mazao ya chikichi na kakao.

## Kicheko ujenzi barabara ya lami

**Na Nebart Msokwa,** ILEJE

WANANCHI wa Wilaya ya Ileje mkoani Songwe, wameanza kufurahia matunda ya barabara ya lami kutoka katika mji wa Isongole wilayani hapa mpaka eneo la Mpemba wilayani Momba yenye urefu wa zaidi ya kilomita 50 ambayo ujenzi wake unakaribia kukamilika.

Wakizungumza na Nipashe jana, baadhi ya wananchi hao walisema barabara hiyo bado haijakamilika, lakini maeneo yote yaliyokuwa korofi yamekamilika na wameanza kunufaika licha ya kwamba baadhi ya maeneo bado haijafunguliwa.

Mmoja wa wananchi hao, Joachim Mwambene, alisema baada ya ujenzi wa barabara hiyo kuanza kukamilika, magari ya abiria yameongezeka na hata nauli imeanza kupungua tofauti na ilivyokuwa kabla ujenzi huo haujaanza.

Alisema nauli kutoka Mpemba mpaka Isongole imepungua kutoka Sh. 5,000 hadi Sh. 4,000 huku akidai kuwa wana matumaini kuwa itapungua zaidi baada ya ujenzi huo kukamilika.

Alisema kwa sasa baadhi ya wamiliki wa magari wameanza kupeleka magari mazuri ya abiria yakiwamo mabasi tofauti na awali, ambapo walikuwa wanategemea magari madogo aina ya Noah.

"Sasa hivi ukichelewa sana basi unatumia masaa (saa) mawili (mbili) kutoka Isongole kwenda Mpemba na ikikamilika tutakuwa tunatumia saa moja tu maana sasa hivi ni maeneo machache ambayo tunapita kwenye lami," alisema Mwambene.

Naye Jailosi Chisunga, alisema kabla ya ujenzi wa barabara hiyo kuanza kuna baadhi ya maeneo yalikuwa makorofi kiasi kwamba magari yalikuwa yanakwama hasa kipindi cha mvua na kwamba asilimia kubwa ya maeneo hayo yametengenezwa.

Alisema eneo ambalo lilikuwa korofi zaidi ilikuwa eneo la Mto Songwe katika eneo la Ikumbilo, ambapo wakati mwingine mto huo ulikuwa unafunga barabara na kukwamisha watu kusafiri lakini kwa sasa pameboreshwa.

Alisema kuanzia katika eneo hilo mpaka Isongole ambapo ni zaidi ya kilomita 10 kwa sasa ni lami na magari yamesharuhusiwa kuanza kupita na hivyo kuwapunguzia adha ya kukwama.

Nao baadhi ya madereva wa magari ya abiria wanaotumia barabara hiyo walidai kuwa kabla ya barabara hiyo kuanza kujengwa magari yalikuwa yanaharibika mara kwa mara kutokana na ubovu wa barabara hiyo.

Mmoja wa madereva hao, Salanga Chuku, alisema walikuwa wanatumia muda mwingi kutengeneza magari yao kuliko kuwa barabarani hali ambayo ilikuwa inawatia hasara.

# Mufti aonya athari za mitandao katika ndoa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISI ya Mufti Zanzibar imewaonya wanandoa juu ya matumizi ya mitandao na kuheshimiana ili kuendelea kulinda ndoa zao.

Naibu Mufti wa Zanzibar, Sheikh Mahmoud Mussa Wadi, alisema hayo jana katika hafla ya kuwatunuku vyeti wahitimu 24 wa mafunzo ya ndoa Kisiwani Pemba.

Alisema Ofisi ya Mufti kila siku hupokea malalamiko ya wanandoa ambayo huchangiwa na matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii kwa wanandoa.

**Wanapohojiwa hueleza jinsi mmoja ya wanandoa anavyoitumia mitandao ya kijamii kwa usiri mkubwa.**

Naibu Mufti alisema wanapohojiwa hueleza jinsi mmoja ya wanandoa anavyoitumia mitandao ya kijamii kwa usiri mkubwa.

Sheikh Mahmoud alisema kuwa ulimwengu wa sasa kila mmoja ana simu inayomwezesha kuwasiliana na mtu kwa njia yoyote, lakini wako wanaokosa maadili kwa kuitumia vibaya.

Aliwataka wanandoa kuishi kwa kuaminiana na kuitumia mitandao hiyo kwa njia ya kujifunza.

Pia aliwataka wahitimu hao wa mafunzo ya ndoa kuwa mfano mzuri katika ndoa zao na jamii kwa ujumla ili elimu ya ndoa waliyoipata izae matunda.

Kadhalika, aliwataka wanandoa kulinda ndoa zao, ili kusijitokeze talaka holela na kuishi kwa upendo ili kuwa fundisho kwa watu wengine.

Naye mkufunzi wa mafunzo hayo, Said Ahmed Mohamed, alisema anaamini wanafunzi hao watakuwa waaminifu katika ndoa zao.

Akisoma risala kwa niaba ya wahitimu wenzake, alisema elimu waliyoipata imewapa uwelewa wa elimu ya ndoa ikiwamo kumtunza mke au mume.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman (kushoto), akizungumza na Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi nafasi ya Rais, Juma Ali Khatib (kulia) pamoja na Mwakilishi wa Jimbo la Mwera, Mihayo Juma Nhunga, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Bei ya petroli yapaa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), imefanya mabadiliko ya bei za mafuta Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi ofisini kwake Maisara, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano, Mbarak Hassan Haji, alisema mafuta ya petroli kwa mwezi huu yamepanda kutoka Sh. 1,918 mwezi uliopita na kufikia Sh. 1,948.

Mbarak alisema mafuta ya diseli yameshuka kutoka Sh. 1,901 mwezi uliopita hadi 1,866 sawa na asilimia 1.84

Kwa upande wa mafuta ya taa, Mbarak alisema bei ya rejareja imebaki ile ile ya mwezi uliopita ambayo ni Sh. 1,606.

Akizungumzia mafuta ya meli (banka), alisema kwa sasa ZURA haipangi bei za mafuta hayo, kutokana na kutotumiwa na wananchi na badala yake kuwaachia wenyewe zikiwamo kampuni kama wanavyofanya Tanzania Bara.

"Tumeona sisi sasa hivi tusipange bei ya mafuta ya ndege kwani mafuta haya hawatumii wananchi binafsi zaidi yanatumiwa na kampuni za ndege kubwa," alisema.

Sababu zilizofanya kupanda kwa bei ya petroli, alisema, ni kutokana na kubadilika kwa wastani wa bei za uuzaji wa bidhaa hizo katika soko la dunia pamoja na soko la ndani kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

Aliwahimiza wananchi kuwa bei zilizotangazwa na serikali ndizo halali na kuwataka kununua mafuta katika vituo halali na kudai risiti pale wanapouziwa nishati hiyo, ili kuepuka kuuziwa mafuta kimagendo au yasiyo salama kwa vyombo vyao.

"Mara chache huwa tunaamua kubadilisha kidogo kulingana na bei halisi hasa pale bei inapopanda sana, ZURA inaamua kufidia hali ili kuepusha kuwatwisha mzigo wananchi," alisema.

Hata hivyo alisema sababu nyingine ni mahitaji ya bidhaa hiyo kuwa kubwa duniani kulinganisha na bidhaa zingine.

Naye Ofisa Uhusiano wa Mamlaka hiyo, Hassan Juma Amour, alisema miezi iliyopita janga la corona lililokumba nchi mbalimbali duniani, lilisababisha bei ya mafuta kushuka na soko la mafuta lilipungua, lakini hivi sasa janga hilo limeanza kupungua duniani na bei imeanza kuongezeka katika soko la dunia kutokana na kuongezeka pia kwa mahitaji.

# Wanawake wasisitizwa kuwa jasiri

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAWAKE wametakiwa kuwa wakakamavu na kutoogopa vikwazo vinavyowakabili katika kugombea nafasi za uongozi.

Hayo yalisema juzi na wajumbe wa Kamati ya Wanaume wa Mabadiliko wakati wakiwasilisha ripoti ya utekelezaji wa majukumu yao yaliofanyika visiwani Zanzibar.

Yussuf Abdallah Ramadhani, mmoja wa wajumbe hao, alisema lengo la kamati hiyo ni kuhakikisha wanapita kila eneo ndani ya jamii kukutana na watu tofauti kuelimisha na kushawishi kuhusu umuhimu na nafasi ya wanawake katika kugombea uongozi.

Alisema lengo la Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Ofisi ya Zanzibar ni kuhakikisha wanaifikia jamii kuwapatia elimu ambayo ni chachu ya kuwabadilisha wanawake kisiasa.

Kwa mujibu wa mjumbe huyo, malengo la kamati yao ni kutekeleza majukumu yao kwa kuwafikia wananchi kuwahamasisha wanawake kujitokeza kugombea nafasi za uongozi.

Naye Amour Rashid, mjumbe wa kamati hiyo, alisema malengo ya TAMWA kuunda kamati hiyo ni kuhakikisha wanawake wanakuwa na mwamko wa kugombea nafasi za uongozi.

Alisema TAMWA imewakomboa wanawake kiuchumi na imekuwa na nyenzo tofauti za kuhakikisha wanajikomboa kiuchumi na kuondokana na umaskini.

"Zipo fursa za uongozi, hivyo ni vyema wanawake kuzitumia na msikubali kusikiliza maneno yasio na tija kwenu na badala yake nafasi hizi kuziacha na kuwachagua wanaume pekee, juweni kwamba hizi fursa ni za kila mtu," alisema.

Aidha, aliwataka wanawake kujitokeza katika kugombea nafasi hizo ikiwa ni pamoja na kujitambua na kulinda heshima pamoja na mipaka ya dini.

Mratibu wa TAMWA Pemba, Fathiya Mussa Said, alizitaka kamati hizo kuendelea kuelimisha jamii ili lengo la upatikanaji wa mabadiliko kwa wanawake yanaonekana.

Pia aliwataka wanawake wanapopata ridhaa za kuchaguliwa kuwa viongozi majimboni, wasisahau majukumu yao na walinde maadili yao.

**Zipo fursa za uongozi, hivyo ni vyema wanawake kuzitumia na msikubali kusikiliza maneno yasio na tija kwenu na badala yake nafasi hizi kuziacha na kuwachagua wanaume pekee, juweni kwamba hizi fursa ni za kila mtu.**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA NA MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA IKO KAHAMA** MAJENGO VYUMBA VITATU INA MAJI NA UMEME, PLOT No 759, BLOCK "E", KIWANJA NI MEDIUM SIZE. MAWASILIANO ZAIDI; 0759359933/0713553819

***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ISACK JOHN DANYESI** Amepotelewa na cheti cha elimu ya kidato cha NNE alichomaliza katika shule ya secondari AGAPE MBAGALA mwaka 2017, chenye Index no: S1523/0086/2017. Kwa yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote Cha polisi rb namba: **MOR/MOR/RB/776972/2020.**

## KUFUNGWA KWA KAMPUNI

Wamiliki wa kampuni ya **ROSARU TANZANIA COMPANY LIMITED** namba ya usajili **138370** ya tarehe **05/10/2017** wanapenda kuutangazia umma kuwa kampuni yao imefilisika na hivyo kuamua kuifunga kwa mujibu wa sheria ya makampuni ya Brela.

115984502

## TANGAZO

### TANGAZO LA KUPOTEA KWA HATI

**ELIETHA NANDUPE SWITI** wa **S.L.P 460, Mpanda** anatangaza kupotelewa na hati ya kiwanja Namba 252 Block "R" kilichopo eneo la **MAKANYAGIO, MPANDA. Title No. 16605-MBYLR.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi au awasiliane kwa namba **0784 909728.**

**Taarifa ya Polisi: KAT/MPA/RB/508664/2020.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya CHAMWINO MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi No. 101/2020.**

**Ombi la SCOLASTICA N. MKANE kuteuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu DAMSON ANDREA MKANE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria shauri wakitaka mnamo tarehe 23/11/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo. Tarehe 09/11/2020.




115990902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;340/2020**

**Ombi la DAVID EMMANUEL HEMBULA,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu EMMANUEL DAUDI HEMBULA .**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 03/12/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 10/11/2020.




115990802

## Amepotelewa na result slip na leaving certificate



**CHRISTIAN L MAHUNDU**

Amepotelewa na result slip na leaving certificate vya kidato cha nne vyenye index namba **S.0181.0045** vilivyotolewa na shule ya secondary **KISARAWE LUTHERAN JUNIOR SEMINARY** mwaka 2019,yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **PWA/KIS/RB/786541/2020**

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJ

**AHAMED MAHAMUD MOHAMED** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJ YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 673 AVH.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **ENG/IR/96/2020.**

115990702

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

Ndg.**SAID RAMADHANI MARUSU** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye maelezo yafuatayo :

Blue kadi namba :

**MC 354 CPA**

Kwa yeyote atakayeiona,anaombwa kuripoti kituo chochote cha polisi kilicho karibu.

**LOSS REPORT NAMBA : MBE/MBA/RB/453820/2020.**

115989802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**MJINI-MOROGORO**

Usimamizi wa mirathi **No;322/2020**

Ombi la **LUBUVA LEONARD MARUSU,**Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **LEONARD STEPHAN MARUSU** .Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo **Tarehe 06/11/2020** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa **Tarehe 22/10/2020.**




**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**MJINI-MOROGORO**

Usimamizi wa mirathi **No;338/2020**

Ombi la **ERICK KINAS SANGA**,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **SARAH YORAM MBOGERA.**Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo **Tarehe 01/12/2020** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa **Tarehe 09/11/2020.**




## TANGAZO

### SIKU YA MAPACHA - TWINS DAY 11 NOVEMBER

EDEN COMMUNITY CENTRE FOUNDATION wanawakaribisha wote kuja kusherehekea pamoja na WATOTO MAPACHA (TWINS) tarehe 11/11/2020 kwenye KITUO CHA EDEN, KIBAHA MISUFINI kuanzia saa 6:00 mchana hadi saa 10:00 jioni. Kwa mawasiliano: JOY DANIEL 0767 562452 au HOSSANA DANIEL 0657 382803.
**WOTE MNAKARIBISWA.**

## TANGAZO

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**OKOKA E. SANGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 222 AHT.** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**TAARIFA YA POLISI: MBE/MBE/RB/780778/2020.**

***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa Kwa***

***Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA



Mwanasheria Mkuu wa Marekani, William Barr (kushoto) na Rais Donald Trump katika Ikulu ya White House. **PICHA: ALLIANCE**

# Rais Trump amfuta kazi waziri wa ulinzi

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amemfuta kazi Waziri wa Ulinzi, Mark Esper.

Rais Trump alitoa tangazo hilo jana kupitia ukurasa wake wa kijamii wa Twitter, kueleza kuwa Christopher Miller, ambaye ni mkuu wa sasa wa kituo cha kukabiliana na ugaidi amechukua nafasi hiyo.

Uamuzi huo umetokana baada ya wawili hao kutofautiana hadharani katika wiki za hivi karibuni.

Rais Trump mpaka sasa hajakubali kushindwa na Rais mteule Joe Biden katika uchaguzi mkuu uliofanyika mwishoni mwa wiki. Ameapa kupinga matokeo hayo mahakamani.

Wiki chache zilizosalia kabla ya Biden kuchukua ofisi Januari 20, Trump bado ana uwezo wa kufanya maamuzi.

Miller alionekana akiingia makao makuu ya kitengo cha ulinzi Pentagon siku ya Jumatatu muda mfupi kabla ya Rais Trump kutangaza kufutwa kwake.

Ofisa huyo wa zamani wa vikosi maalum, alidumu katika Baraza la Usalama la Kitaifa la Rais Trump kabla ya kuwa mkuu wa kituo cha kukabiliana na ugaidi Agosti, mwaka huu.

Katika barua ya kuacha kazi, Esper aliwashukuru maofisa wa vikosi vya jeshi na kusema kwamba, anajivunia yale aliyoweza kufikia katika kipindi cha miezi 18 alichohudumu Pentagon.

"Nilihudumia nchi yangu kwa mujibu wa katiba, kwa hivyo nakubali uamuzi wako wa kumleta mtu mwingine kuchukua nafasi hii," aliandika Miller.

Mwanasiasa wa ngazi ya juu wa Chama cha Democratic, Nancy Pelosi, amekosoa uamuzi huo.

"Kufutwa ghafla kwa Waziri Esper ni ishara wazi kwamba Rais Trump ana lengo la kutumia siku zake za mwisho ofisini kuvuruga demokrasia ya Marekani na sehemu nyingine duniani," alisema Pelos ambaye ni Spika wa Bunge la Wawakilishi.

**"Kufutwa ghafla kwa Waziri Esper ni ishara wazi kwamba Rais Trump ana lengo la kutumia siku zake za mwisho ofisini kuvuruga demokrasia ya Marekani na sehemu nyingine duniani," alisema Pelos ambaye ni Spika wa Bunge la Wawakilishi.**

Kwa nini walitofautiana?

Esper alitofautiana na Rais Trump kufuatia mwenendo wa White House kwa majeshi wakati wa maandamano dhidi ya ubaguzi wa rangi mapema mwaka huu.

Wakati Marekani ilipokumbwa na maandamano makubwa kufuatia kifo cha mtu mweusi, George Floyd, mikononi mwa polisi mjini Minneapolis, Minnesota, Mei, Rais Trump alitishia kutumia wanajeshi kuvunja maandamano hayo.

Juni, Esper, ofisa wa zamani wa jeshi alisema hakuna haja ya kutumia jeshi, tamko ambalo linasadikiwa halikuridhisha White House.

Kufuatia tofauti hizo, kulikuwa na fununu kwamba Rais Trump huenda akamfuta kazi Waziri wa Ulinzi, japo siku ya Jumatatu Trump hakutoa sababu ya kumfuta.

Esper pia ametofautiana na Rais Trump kuhusu hatua ya Rais Trump kulipuuza Shirika la Kujihami la nchi za Magharibi (NATO).

Katika mahojiano na gazeti la Military Times wiki iliyopita, Esper alisema licha ya kuwa na uhusiano mgumu na White House, hakuamini kuondoka ni hatua nzuri.

"Rais amekuwa wazi kuhusu kile anachotaka. Na amekuwa wazi kuhusu maoni yake... sijaribu kumfurahisha mtu yeyote," aliuambia mtandao huo na kuongeza:

"Kile ninachojaribu kufanya ni kutimiza anachotaka, kwa sababu amechaguliwa na ndiye kamanda mkuu wa majeshi."

Rais Trump amewafuta kazi maofisa kadhaa na washauri wakati wa utawala wake, mara nyingi kupitia ujumbe wa Twitter.

Mtangulizi wa Esper alikuwa James Mattis, ambaye alijiuzulu mwaka 2018 baada ya kutofautiana na Rais Trump kuhusu masuala tofauti ikiwamo vita vya Syria.

Wakati wa maandamano ya Juni, dhidi ya ubaguzi wa rangi, Mattis alimkosoa Rais Trump akisema: "Ni rais wa kwanza katika maisha yangu ambaye hataki kujaribu kuunganisha watu wa Marekani - wala hajifanyi kuwa anajaribu. Badala yake anajaribu kutugawanya".

***BBC***

# Mvutano kutishia muungano serikali ya Rais Tshisekedi

**KINSHASA, Congo**

VYAMA vinavyomuunga mkono Rais mstaafu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Joseph Kabila, maarufu FCC, vimeionya muungano wa CACH unaomsapoti Rais Felix Tshisekedi, kuhusu jaribio lolote la kuvuruga bunge la taifa ili kujitafutia uwingi bungeni.

Katika taarifa iliyotangazwa baada ya mkutano wa kisiasa wa siku mbili, FCC imetaka kuandaliwe uchaguzi wa mapema kwenye ngazi zote, ili kuwapa mamlaka raia ya kuamua. Tangazo hilo limekuja wakati Rais Tshisekedi akiendelea na mikutano yake ya mashauriano kwa lengo la kuunda umoja wa kitaifa.

Mwishoni mwa wiki muungano wa FCC ulimaliza mkutano wake wa kisiasa na baadaye ukatangaza msimamo wake.

FCC inayoongoza nchi kwa ushirikiano na CACH, muungano unaoongozwa na Rais Felix Tshisekedi, imearifu kwamba ipo tayari kuzungumza naye Rais Tshisekedi, ila yote yafanyike kufuatana na mpango wa mkataba waushirikiano.

"FCC inafuatilia kwa makini namna mikutano ya mashauriano iliyoanzishwa naye Rais Tshisekedi inavyoendeshwa, na inajulisha msimamo wake. Yaani, FCC ipo tayari kwa mazungumzo naye rais, ikiwa yatafanyika kama ilivyopangwa na mkataba wa ushirikiano," alisema Mratibu wa FCC, Nehemie Mwilanya.

Mbali na hilo, mambo mengine ambayo FCC imeyaonya pamoja na rushwa, ambayo imedai inatolewa na muungano wake Rais Tshisekedi kwa mabunge ili kukubali wajiunge na CACH, pia tishio la kulifuta bunge la taifa. Aidha, FCC imesisitiza kwamba ipo njia moja tu ya kujipatia uwingi bungeni, nayo ni kupitia uchaguzi na ndiyo maana, muungano wake Joseph Kabila umesema upo tayari kwa uchaguzi wa mapema kwenye ngazi zote.

Wito huo wa uchaguzi ni jambo lisilokubalika upande wa Muungano wa Demokrasia na Maendeleo ya Jamii (UDPS), chama chake Rais Felix Tshisekedi.

Kiongozi wa muungano wa vijana wa chama hicho, Ted Beleshay, alieleza kwamba kutakuwa kwanza na mageuzi kabla ya uchaguzi.

"Sisi tunawaza kupaswa kuwe na mageuzi katika tume ya uchaguzi, pia mageuzi ya sheria ya uchaguzi. Tunao muda hadi mwaka 2023 kwa kufanya hayo, ili tuwe na tume itakayotoa matokeo yasiyo na mabishano. Kufuta bunge, mambo hayo yapo chini ya katiba kama alivyoeleza rais, ila kwa kweli hiyo ni hatua ya mwisho," alisema Beleshay.

Wakati huu, Rais Tshisekedi anaendelea na mikutano ya mashauriano kwa muda wa wiki moja sasa. Hadi sasa ni FCC, yaani muungano wake Rais mstaafu Joseph Kabila ndio unao wingi wa viti vya wabunge bungeni.

**DW**

# MAKOCHA

## EPL WATAKA 'SAB' WACHEZAJI WATANO




**LONDON, England**

MAKOCHA wa klabu za Ligi Kuu ya England wanaweza kuomba kurudishwa kwa kanuni ya matumizi ya idadi ya wachezaji wa akiba kufikia watano.

Ongezeko la idadi ya makocha wanaotaka kanuni hiyo kurudishwa ndio linatoa picha kuwa huenda mpango huo ukarejea kama ilivyokuwa mwishoni mwa msimu uliopita kutokana na janga la corona.

Ligi Kuu ya England (EPL), ndio pekee ambayo ilirudisha matumizi ya wachezaji watatu wa akiba au mfumo wa awali.

Baadhi ya makocha wanaamini kuwa ongezeko la majeruhi linachangiwa na ufinyu wa wachezaji wa akiba kwani wachezaji hao wanatakiwa kucheza michuano mingi kwa muda mfupi ilhali hawapati nafasi ya kupumzika.

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp, na mwenzake wa Manchester City, Pep Guardiola wote baada ya mchezo wao wa Jumapili kumalizika walionyesha kutofurahishwa na mfumo wa kutumia wachezaji watatu pekee wa akiba.

Kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer ana madai yanayoendana na hayo kwani analalamikia ugumu wa ratiba kati ya mchezo mmoja hadi mwingine ambapo alisafiri na kikosi chake cha United kwenda Uturuki kabla ya mechi ya Everton.

Kocha wa West Ham United, David Moyes anasema awali alikuwa anaupinga mfumo huo, lakini sasa yuko tayari kuupigia chapuo kurejea.

Changamoto kubwa ambayo makocha wanaosapoti mfumo huo wanakutana nayo ni kuwa ili kanuni hiyo irudi inabidi kura zipigwe na hapo kwenye kura ndipo zinapoanguka, klabu nyingi ndogo zinapinga matumizi ya wachezaji watano wa akiba.



## MAN CITY, LIVERPOOL GONJWA MOJA - NEVILLE

**LONDON, England**

GARY Neville amesema kwamba, timu mbili za Manchester City na Liverpool ni dhaifu zaidi msimu huu baada ya sare ya 1-1 pale Etihad, Jumapili.

Timu hizo zinazonolewa na kocha, Pep Guardiola na Jurgen Klopp, zimekuwa zikipambana kileleni mwa msimamo wa Ligi ya Kuu kwa misimu miwili iliyopita na City ikiwachapa 'Wekundu' hao msimu wa 2018-19 kabla Liverpool kumaliza miaka yao 30 ya kusubiri taji la ligi mapema mwaka huu.

Lakini Neville, akizungumza baada ya kutoa maoni juu ya mechi ya Jumapili, anaamini wote kwa sasa hawapo katika kiwango sawa.

Liverpool tayari imeruhusu mabao 16 katika michezo nane wakati Man City imefanikiwa kufunga mara 10 tu, idadi ya chini ikilinganishwa na kuanza kwao kwa bao la bure kwenye msimu iliyopita chini ya Pep Guardiola.

Neville alisema ukosefu wa mabao ya City ni kwa sababu ya kukosekana kwa mshambuliaji, Sergio Aguero.

Muargentina huyo amecheza mara tatu tu msimu huu kwa sababu ya shida za magoti na misuli.

"Hakika Manchester City wanashida, kwa sababu wanategemea sana mchezaji mmoja," alisema Neville akiiambia Sky Sports.

## ETO'O CHUPUCHUPU KUPOTEZA MAISHA



**YOUNDE, Cameroon**

NYOTA wa zamani wa Barcelona na Cameroon, Samuel Eto'o, amelazwa hospitalini baada ya kupata majeraha kichwani kutokana na kupata ajali ya gari nyumbani kwao Cameroon.

Kwa mujibu wa France Football, mshambuliaji huyo aliyewahi kuzichezea pia Inter Milan, Chelsea na Everton alihitaji kufanyiwa vipimo zaidi baada ya gari yake kugongana na basi.

Ajali hiyo imetokea karibu na mji wa Nkongsamba huko Cameroon, wakati Eto'o akiwa anaendesha akitoka kwenye sherehe ya harusi.

Mwandishi wa habari, Martin Camus, alizungumza na Eto'o ambaye alitaka kuwaondoa hofu watu kwa kuwahakikishia kwamba anaendelea vizuri.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo ya BBC, hakuna kifo chochote kilichoripotiwa kwenye ajali hiyo baada ya kuzungumza na moja ya ndugu wa mwanasoka huyo.

Eto'o alistaafu soka mwaka mmoja uliopita baada ya kupata mafanikio makubwa akipita kwenye timu kibao ikiwamo Real Madrid, Barcelona, Inter Milan na Chelsea kwa kuzitaja kwa uchache huku akibeba mataji mengi ikiwamo matatu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Alibeba pia medali ya Dhahabu ya Olimpiki na alishinda ubingwa wa Afcon akiwa na kikosi cha Cameroon mwaka 2000 na 2002.

## HABARI MICHEZO



# LOW AWATEMA
## MULLER, BOATENG NA HUMMELS

**MUNICH, Ujerumani**

KOCHA Mkuu wa Ujerumani, Joachim Low, ameondoa uwezekano wa kuwaita wachezaji wazoefu kwenye mechi za kimataifa, nyota wawili wa Bayern Munich, Thomas Muller na Jerome Boateng pamoja na mkali wa Borussia Dortmund, Mats Hummels.

Low aliwatema wachezaji hao watatu kuanzia Machi 2019 wakati akiangalia namna ya kukijenja upya kikosi cha Ujerumani baada ya kuwa na matokeo mabaya kwenye Kombe la Dunia mwaka 2018.

Kiungo mshambuliaji, Muller (ana mechi 100), na walinzi Boateng (mechi 76) na Hummels (mechi 70) kwa pamoja wamecheza jumla ya mechi 246 kwa Ujerumani na walishinda Kombe la Dunia mwaka 2014, lakini kwa sasa wana umri wa zaidi ya miaka 30.

Na Low amebainisha kwamba, kwa sasa hana mpango wa kuwaita nyota hao katika kikosi chake, labda kuwe na hali ya dharura.

"Tumekubaliana kutowaita wachezaji hawa watatu, hakuna kilichobadilika," alisema Low akiliambia gazeti la Kicker.

"Hatuwezi kurudi nyuma. Wao ni wachezaji wakubwa na wa daraja la juu, lakini kwa sasa nafasi yao haipo tena."

## MARTINEZ AIBEZA ARSENAL, AJISIFIA KUTUA ASTON VILLA

**LONDON, England**

KIPA Emiliano Martinez anaamini kutua kwake Aston Villa akitokea Arsenal ilikuwa "hatua nzuri" wakati akiendelea kung'ara na klabu yake hiyo mpya.

Martinez alijiunga na Villa akitokea Arsenal Septemba mwaka huu kwa ada iliyoripotiwa kuwa ni pauni milioni 20.

Baada ya kutoruhusu bao kwenye mchezo wa Villa wakati wakiwafunga Arsenal 3-0 kwenye Ligi Kuu Jumapili, Martinez amesema uhamisho huo umekuwa hatua nzuri kwenye maisha yake kisoka.

"Wakati nilipoamua kuja Villa ilikuwa kwa sababu niliamini nia ya kocha, niliamini malengo ya klabu na nilijua namna gani Villa ilivyo kubwa.

"Watu hawajua namna gani Aston Villa ilivyo kubwa," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Walisema kwamba nimerudi chini katika maisha yangu kisoka na mara zote nilisema hii ni hatua nzuri zaidi kwa maisha yangu.





"Tunakwenda kuwa na msimu bora zaidi, tunaendelea kupambana katika kila mechi, kwa kila mpira, na matumaini yangu tutakuwa kwenye nafasi nzuri kabisa kwenye msimamo."



## PJANIC AWEKA WAZI KUTOICHEZEA UFARANSA

**BARCELONA, Hispania**

MIRALEM Pjanic amedai kwamba, alipewa ofa ya kuichezea timu ya Taifa ya Ufaransa, lakini ingekuwa ni sawa na kuvunja moyo wake kuikacha Bosnia-Herzegovina.

Kiungo huyo wa Barcelona alizaliwa jijini Tuzla, Bosnia-Herzegovina wakati huo ikiwa chini ya Yugoslavia, kabla ya familia yake kuhamia nchini Luxembourg muda mchache baada ya kulipuka kwa vita ya Bosnian.

Pjanic aliichezea timu ya Taifa ya Vijana ya Luxembourg na akasajiliwa na Klabu ya Metz ya Ufaransa akiwa na umri wa miaka 14, kabla ya kutua Lyon.

Na wakati akicheza kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, aliyekuwa kocha mkuu wa timu ya taifa, Raymond Domenech, alimwomba kuichezea timu hiyo.


"Ndio, ningeweza kuichezea timu ya Taifa ya Ufaransa wakati nilipotua Lyon, lakini nilisema siku chache kabla kuwa ndoto yangu ni kuipigania Bosnia," alisema Pjanic mwenye umri wa miaka 30, akiiambia Canal Plus.

"Domenech aliniita, lakini tayari nilishafanya uamuzi wangu. Nilimshukuru, lakini nilimwambia ukweli.

"Kwa upande wangu kuichezea Ufaransa, ingekuwa ni sawa na kuuvunja moyo wangu. Na kwa upande mwingine, Bosnia wangeumia zaidi kuniona nikichezea Ufaransa."

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# POGBA HARIDHISHWI UNITED - DESCHAMPS

Kuna nyakati mambo yanakuwa magumu na unaona sehemu uliyopo haina maana tena, hivyo ndivyo...

**PARIS, Ufaransa**

KOCHA Mkuu wa Ufaransa, Didier Deschamps, amebainisha kwamba Paul Pogba haridhishwi na "hali" pale Manchester United baada ya kuwa kwenye wakati mgumu wa kurudisha kiwango chake.

Pogba amecheza mechi 11 kwa United katika mashindano yote msimu huu, lakini ni tano kati ya hizo ndio alianza na tatu zilikuwa za kipigo, ikiwamo ile ya kunyanyaswa kwa mabao 6-1 na Tottenham.

Pogba kwa kawaida alikuwa akicheza pale United kama mshambuliaji wa tatu, na alionyesha kiwango bora kabisa, lakini msimu huu ametengeneza nafasi mbili tu za kufunga kwenye Ligi Kuu, akiwa anacheza kiungo mkabaji.

Deschamps amedai kwamba, Pogba hawezi kuwa na furaha na maisha ya pale United, lakini akabainisha anaweza kujisaidia yeye mwenyewe.

"Sina ushauri," alisema Deschamps kabla ya mchezo wa leo Jumatano wa kirafiki kati ya Ufaransa na Finland.

"Namjua vizuri sana na analijua kundi lile vizuri.

"Kwa hali aliyonayo pale klabuni kwa sasa, hawezi kuridhika nayo na hasa muda wa kucheza na nafasi anayocheza.

"Anahitaji kutafuta muda wa kurudi kwenye ubora wake. Amekuwa akicheza vizuri awali, lakini hatuwezi kumsaidia kufanikisha kile anachotaka.

"Kuna nyakati mambo yanakuwa magumu kwa hali fulani na unaona kabisa sehemu uliyopo haina maana tena, na hivyo ndivyo ninavyoona mambo yanavyokwenda kwa Pogba.

"Kama nilivyosema sina ushauri kwake, lakini kama kijana wangu namuona namna hali ilivyo ngumu kwake na wazi kabisa haridhishwi."

## KWA UFUPI

**ERIKSEN ATAKIWA TENA SPURS**
KLABU ya Tottenham imempa ofa ya kumsajili tena kiungo wa Denmark, Christian Eriksen, mwenye umri wa miaka 28, kutoka Inter Milan. ***(Football Insider)***

**GIROUD AFIKIRIA HATIMA YAKE**
OLIVIER Giroud anafikiria majaliwa yake pale Chelsea, huku mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 34, akihusishwa na Inter Milan. ***(Football London)***

**FATI ABEBA DEMBELE BARCA**
MANCHESTER United inaweza kumkosa Ousmane Dembele katika usajili wa Januari, huku Barcelona wakijiandaa kumpa nafasi zaidi nyota huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 23, baada ya kuumia kwa Ansu Fati. ***(Sport - in Spanish)***

**BALE APEWA OFA MPYA**
TOTTENHAM inaweza pia kumpa ofa ya kumsajili nyota wa Wales, Gareth Bale, mwenye umri wa miaka 31, kwa mkataba wa kudumu kutoka Real Madrid, kwa ada inayotajwa kuwa euro milioni 15. ***(Mundo Deportivo)***

**UNITED WAMBANIA ROMERO**
KLABU ya Manchester United inasita kutoa uamuzi kwa golikipa wake, Sergio Romero, mwenye umri wa miaka 33 raia wa Argentina, hadi wakamilishe maendeleo ya Dean Henderson, kwani kuna uwezekano kwa nyota huyo wa England mwenye umri wa miaka 23, kuondoka Januari kwa mkopo. ***(ESPN)***

**AHMEDHODZIC BADO CHELSEA**
JARIBIO la Chelsea kutaka kumsajili mlinzi wa zamani wa Nottingham Forest, Anel Ahmedhodzic, kutoka Malmo limezuiwa, kwa mujibu wa baba mzazi wa nyota huyo mwenye umri wa miaka 21 raia wa Bosnia. ***(Sun)***

**LINDELOF AZUIWA UNITED**
MANCHESTER United imemzuia mlinzi wake, Victor Lindelof, mwenye umri wa miaka 26, kujiunga na kikosi cha Sweden kinachojiandaa na mchezo wa kirafiki dhidi ya Denmark kwa sababu ya corona. ***(Goal)***

**LIVERPOOL YAFUNGA UWANJA**
LIVERPOOL imefunga mlango kwa mara ya mwisho kwenye uwanja wao wa mazoezi walioutumia kwa zaidi ya miaka 60 wa Melwood. ***(Liverpool Echo)***

**WEST HAM YAPEWA SOMO**
MLINZI wa kushoto wa England, Aaron Cresswell, mwenye umri wa miaka 30, anataka West Ham kuijenga upya timu hiyo. ***(London Evening Standard)***

**SONG KUJAZWA NOTI SPURS**
MMLIKI wa Klabu ya Tottenham Hotspur, Joe Lewis, ameruhusu mshambuliaji wa Korea Kusini, Song Heung-min mwenye miaka 28, kupewa mkataba wenye thamani ya pauni 200,000 kwa wiki na marupurupu mengine. ***(Football Insider)***

**DALOT ATAKIWA JUMLA MILAN**
AC Milan inajaribu kuangalia kama Manchester United itakuwa tayari kumuuza kiungo wake wa kimataifa wa Ureno chini ya umri wa miaka 21, Diogo Dalot, baada ya kucheza kwa mkopo na klabu hiyo. ***(Tuttosport, via Inside Futbol)***

## HABARI MICHEZO

# KVZ YAANZA KUWASOMA WASUDAN MICHUANO CAF

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya timu ya KVZ kupangwa kucheza na El Amal ya Sudan katika michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika raundi ya awali, Kocha Mkuu wa miamba hiyo ya Zanzibar, Shekha Khamis, amesema tayari ameanza kuwafuatilia wapinzani wao ili kuona namna gani wataweza kukabiliana nao katika michuano hiyo.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa juzi na waandaaji wa michuano hiyo, Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), timu hizo zitakutana kati ya Novemba 27-29, na kurudiana kati ya Desemba 4-6, mwaka huu, KVZ ikianzia ugenini.

Na kwa upande wa Ligi ya Mabingwa Afrika, tarehe hizo pia zitawahusu pia mabingwa wa Zanzibar, Mlandege SC ambao wataanzia nyumbani dhidi ya mabingwa wa zamani wa michuano hiyo, CS Sfaxien ya Tunisia.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa KVZ, Khamis alisema tayari ameanza kuwafuatilia na ana uhakika wanaweza kuwatoa wapinzani wao hao na kusonga mbele hatua inayofuata.

Alisema kuanza ugenini kwa upande wao ni kitu kizuri kwani watakuwa na nafasi ya kuhakikisha wanafanya vizuri mechi hiyo kabla ya kurejeana nyumbani. "Nimejaribu kuwafuatilia wapinzani wetu kwa kuangalia mechi zao mbalimbali katika mitandao na historia yao, ni timu nzuri, cha muhimu kwetu sisi ni kuendelea kujipanga ili tupate nafasi ya kusonga mbele na sio kushiriki tu," alisema.

Alisema timu yake inaendelea na mazoezi kuelekea michuano hiyo ya kimataifa pamoja na Ligi Kuu Zanzibar ambayo inaanza Novemba 14, mwaka huu.

Ili kuendelea kujipanga zaidi, alisema anatarajia kucheza tena mechi ya kirafiki dhidi ya Simba na Yanga za Tanzania Bara ili kukiweka kikosi chake katika hali ya ushindani.




Mkurugenzi wa Kampuni ya Jackson Group Sports, Kelvin Twissa (katikati), akiwatambulisha mabondia, Hassan Mwakinyo (kulia) na Muargentina Jose Carlos Paz ambao watapambana ulingoni Ijumaa katika ukumbi wa Next Door Arena, Oysterbay jijini Dar es Salaam. Siku hiyo Mwakinyo atatetea mkanda wake wa uzito wa Super welter wa mabara unaotambuliwa na Chama cha WBF. **MPIGAPICHA WETU**

# Mwakinyo kumchapa Muargentina kwa KO

**Na Mwandishi Wetu**

BONDIA Hassan Mwakinyo na Muargentina Jose Carlos Paz, wametamba kila mmoja atamchapa mwenzake katika pambano la kuwania ubingwa wa uzito wa super-welter wa mabara unaotambuliwa na Chama cha WBF.

Mwakinyo na Paz watapambana Ijumaa kwenye Ukumbi wa Next Door Arena jijini Dar es Salaam katika pambano la raundi 12.

Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari jana, jijini Dar es Salaam, Mwakinyo alisema atahakikisha Paz anaachana na mchezo wa ngumi za kulipwa kutokana na kipigo cha KO alichumwandalia.

"Natamani pambano lifanyike mapema iwezekanavyo, hata siku moja kabla kwani nipo fiti zaidi ya nilivyokuwa mwanzoni. Sitaki kuwanyong'onyesha Watanzania katika pambano hilo," alisema Mwakinyo.

Alisema anajua Paz ni bondia mzuri na amejiandaa vema katika pambano hilo, lakini kutokana na jinsi alivyojiandaa, hatakuwa na nafasi ya kutamba kwake.

Kwa upande wake, Paz alisema kuwa hakuja nchini kutembea zaidi ya kuwania ubingwa anaoushikilia Mwakinyo.

"Nipo vizuri, mazoezi yangu nchini yamekuwa na mafanikio makubwa na hali ya hewa si tatizo. Nitamfundisha ngumi Mwakinyo," alisema Paz.

Wakati mabondia hao wakitambiana, pia bondia Hussein Itaba na mpinzani wake kutoka DR Congo, Alex Kabangu watapanda ulingoni siku hiyo sambamba na Fatuma Zarika dhidi ya Mzimbabwe Patience Mastara huku Mtanzania Zulfa Macho yeye akizichapa na Mzambia Alice Mbewe.

Mkurugenzi wa Jackson Group Sports, Kelvin Twissa, alisema kuwa maandalizi yote yamekamilika na kuwaomba mashabiki kuendelea kununua tiketi kwa ajili ya pambano hilo.

"Maandalizi yapo vizuri na kama mnavyoona mabondia wote wapo hapa na sasa tunamsubiri Rais wa EBF, Howard Goldberg na mwamuzi Edward John Marshall ambao watawasili leo, Jumatano," alisema Twisa.

Twissa alisema tiketi zitaanza kuuzwa kwa njia ya Nilipe na Selcom kwa Sh. milioni tatu kwa meza ya watu 10 na Sh.150,000 kwa viti vya kawaida.

## Namungo: Ligi Kuu imetuweka fiti CAF

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Klabu ya Namungo, Hitimana Thierry, amesema michezo ya Ligi Kuu waliyocheza imesaidia kuwaweka sawa wachezaji wake kuelekea michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika wakati huu ratiba ya kinyang'anyiro hicho ikionyesha watakutana na Al Rabita FC ya Sudan Kusini wakianzia nyumbani kati ya Novemba 27-29 kabla ya kurudiana ugenini kati ya Desemba 4-6, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, kocha huyo, alisema haihofii timu hiyo kutokana na mazoezi na mbinu anazowapa wachezaji wake kupitia mechi za Ligi Kuu walizocheza hadi sasa wakati huu ligi hiyo ikielekea raundi ya 11.

Alisema alikuwa anasubiri kwa muda mrefu ratiba hiyo ili kufahamu wapinzani wao.

"Kwa upande wangu nimefurahi kujua timu ambayo nitakutana nayo kwenye Kombe la Shirikisho, lengo langu ni kusonga mbele," alisema Hitimana.

Alisema wachezaji wote wanaendelea vizuri na mazoezi na kwa upande ya waliokuwa majeruhi wanaendelea vizuri pia.

Kuhusu ubora wa wapinzani wao, Hitimana alisema, baada ya ratiba hiyo kutoka, amewafuatilia kupitia mtandao na kubaini sehemu ambazo ni dhaifu, hivyo kinachotakiwa kwa sasa ni pamoja na sala za Watanzania.

## Riadha Singida yapata viongozi

**Na Jumbe Ismailly, SINGIDA**

JUMA Mataka amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Riadha Mkoa wa Singida kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia sasa, baada ya kuibuka kidedea katika mkutano mkuu wa uchaguzi wa chama hicho uliofanyika juzi mkoani hapa.

Akitangaza matokeo ya uchaguzi huo uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa huo, Ofisa Maendeleo ya Michezo Mkoa wa Singida, Henry Kapera, alifafanua kuwa Mataka aliibuka kidedea baada ya kupata kura 16 kati ya 22 zilizopigwa na kuwashinda wapinzani wake watatu wa kwenye nafasi hiyo.

Kapera alisema Mataka alimbwaga aliyekuwa Mwenyekiti aliyemaliza muda wake, Rashidi Itembe ambaye alipata kura tano huku mshindani wake mwingine, Ally Jumbe akiambulia kura nne, huku kwa upande wa nafasi ya Makamu Mwenyekiti, Swalehe Irumba akipata kura zote 22 za ndiyo.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, nafasi ya Katibu Mkuu ilinyakuliwa na Joeli Ngingo aliyepata kura 13 akimshinda aliyekuwa akitetea kiti hicho, Benno Msanga ambaye alipata kura tisa na aliyenyakua kiti cha Katibu Msaidizi akiwa ni Boniface Mkoha aliyepata kura za ndiyo 21 na kura moja iliharibika.

Kapera pia alimtangaza Meshack Matandala kuwa Mjumbe wa Mkutano Mkuu Taifa baada ya kupata kura kumi dhidi ya Madai Jambau aliyepata kura nane na Inviolata Nkya aliambulia kura nne, wakati Elipresia Nicodemu alichaguliwa kuwa mweka hazina kwa kura 13 na kumshinda mpinzani wake Liliani Nyiti aliyepata kura tisa, huku Mjumbe wa Kamati ya Utendaji akiwa ni Damiano Mkumbo aliyepata kura za ndiyo 20 na mbili za hapana.

Michezo
Jumatano Novemba 11, 2020
Nipashe



POGBA HARIDHISHWI UNITED - DESCHAMPS HABARI UK 22

TUPO TAYARI...



Baadhi ya wachezaji wa Simba, kutoka kushoto; Shomary Kapombe, Bernard Morrison na Pascal Wawa wanaotarajiwa 'kukinukisha' dhidi ya Plateau United ya Nigeria kwenye mechi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya Novemba 27-29, mwaka huu. **PICHA: MAKTABA**

## MASHABIKI RUKSA STARS VS TUNISIA

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Soka Afrika (CAF), limeruhusu mashabiki kuingia uwanjani kushuhudia mechi ya kuwania kufuzu Afcon 2021 kati ya Taifa Stars na Tunisia, wakati timu hizo zitakaporudiana nchini Novemba 17, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

CAF, imepiga marufuku mashabiki kuhudhuria viwanjani katika mechi zote inazozisimamia kutokana na mlipuko wa virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19.

Lakini kwa upande wa Tanzania kuelekea mechi hiyo ya marudiano, Shirikisho la Soka nchini (TFF), limeeleza kuwa limeruhusiwa kuruhusu mashabiki nusu ya idadi ya uwezo wa uwanja kushuhudia mchezo huo.

"CAF imeelekeza kuwa idadi ya watazamaji watakaoingia kuwa asilimia 50 ya uwezo wa uwanja, TFF inawasiliana na serikali ili kukidhi matakwa ya CAF katika mechi hiyo," ilieleza taarifa iliyotolewa na TFF jana kwa vyombo vya habari.

Taifa Stars ambayo kwa sasa ipo kambini nchini Uturuki, itashuka dimbani Ijumaa nchini Tunisia kuvaana na wenyeji wao hao katika mechi ya kwanza.

# WAJUE WANAIGERIA WA SIMBA CAF

### ●●●Ni kikosi cha wazawa tupu, Rage aonya, Sven asema hawatoki, uongozi kuiangukia TFF, serikali wapiganie mashabiki kushuhudia...

**Na Saada Akida**

WAKATI Simba ikipangwa kucheza mechi ya raundi ya awali dhidi ya Plateau United ya Nigeria, mechi ya kwanza ikitarajiwa kupigwa ugenini kati ya Novemba 27-29, kabla ya kurudiana Desemba 4-6, mwaka huu, wapinzani wao hao si wakutisha sana hasa kutokana na kutocheza mechi ya kimashindano tangu kuibuka kwa mlipuko wa virusi vya corona.

Plateau iliyoanzishwa mwaka 1975 wakati huo ikiitwa JIB Strikers FC, taji lake la kwanza lilikuwa Kombe la Nigeria mwaka 1999 ilipoishinda 1-0 mechi ya fainali dhidi ya Iwuanyanwu Nationale kwa bao la kujifunga la Donatus Iloka na msimu huu imepata nafasi hiyo ya kushiriki Ligi ya Mabingwa kutokana na kuwa kileleni mwa msimamo Ligi Kuu Nigeria wakati ligi hiyo ilipovunjwa baada ya mlipuko wa corona.

Kwenye Ligi Kuu Nigeria ambayo inashirikisha timu 20, wakati ligi hiyo ikivunjwa Plateau ilikuwa na pointi 49 kileleni baada ya mechi 25, hivyo kuangukia bahati hiyo ya kucheza michuano ya CAF.

Ilipanda Ligi Kuu Nigeria msimu wa 2010 –11 kwa kushinda mechi yake ya mwisho dhidi ya Mighty Jets, lakini mwaka uliofuata wakashuka tena daraja na kisha kupanda tena mwaka 2015.

Ni moja ya timu iliyohusishwa na upangaji wa matokeo mwaka 2013, Plateau United Feeders ikiichapa Akurba FC mabao 79 - 0, hatua iliyozisababishia timu hizo na Police Machine FC pamoja na Bubayaro FC kufungiwa kwa miaka 10 huku wachezaji wakifungiwa kucheza soka maisha.

Plateau United ilitwaa ubingwa kwa mara ya kwanza mwaka 2017, ikiwa chini ya kocha Kennedy Boboye huku mafanikio yake mengine yakiwa ni kutwaa Kombe la Nigeria (FA Cup) mwaka 1999, kutinga fainali ya FA mwaka 1993, 1998.

Kwa upande wa michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, imeshiriki mara moja mwaka 200 na kuishia raundi ya kwanza, huku Ligi ya Mabingwa pia ikishiriki mara moja mwaka 2018.

Kikosi cha timu hiyo kinaundwa na Wanaigeria watupu huku kikitumia uzi wa njano kikiwa nyumbani, ugenini jezi ya kijani na jezi yao ya tatu ni nyeupe.

Akizungumzia mechi hiyo, Kocha wa Simba, Sven Vandenbroeck amesema watashinda na kusonga mbele kwa kuwa mikakati na mipango yao ni kuhakikisha wanashinda na si mchezo huo tu wa awali bali timu kufanya vizuri kufika nusu fainali.

"Tupo tayari kukabiliana na wapinzani wetu, licha ya changamoto ya wenzetu (kutocheza ligi kutokana na corona], lakini kikubwa ni kuhakikisha tunapambana kufanya vizuri katika mechi hiyo kwa kufikia malengo yetu ya kucheza nusu fainali ya michuano hiyo," alisema Sven.

Lakini Mwenyekiti wa zamani wa Klabu ya Simba, Ismail Aden Rage, yeye amesema pamoja na kutopangiwa timu ngumu sana, lakini wasiidharau kwani timu za Nigeria ni ngumu hasa zinapokuwa kwao, hivyo wanatakiwa kujiandaa kimpira na kutafuta namna ya kuwaathiri kisaikolojia wapinzani wao ambao huamini sana mambo ya kishirikina.

"Unapocheza Nigeria, waamuzi wake mara nyingi wanatoka ukanda ule ule wa Afrika Magharibi. Wale jamaa wana ushirikiano sana, hivyo lazima mechi ikichezwa ugenini wajue waamuzi hawatokuwa upande wao kabisa, hivyo wawe makini," alisema Rage.

Kuhusu CAF kuzuia mashabiki kuingia viwanjani katika mechi zake kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah 'Try Again', amesema: "Tumeona ratiba jana (juzi) jioni, ni mapema sana kuzungumza chochote hadi hapo tutakapokutana viongozi kuweka mikakati yetu, tutaomba msaada kwa kuandikia barua Shirikisho la Soka nchini (TFF) kuiomba serikali ieleze CAF usalama wa nchi yetu kuhusu janga hilo."

Kwa upande wa TFF kupitia Ofisa Habari wake, Cliford Ndimbo alisema: "Hatuwezi kuliweka wazi hilo, kwa sababu hata tamko hilo lilipotoka kwa timu ya Taifa, 'Taifa Stars' tulitulia na kuanza kujadili kupitia vikao vya ndani, nadhani hata hilo la Simba na Namungo likifika muda wake litatolewa taarifa," alisema Ndimbo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042